

## **ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

### **SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/“Waziri Kivuli”–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni	Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.

21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Abass Juma Muhibi	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa

	na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Haji Faki Shaali	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Said Ali Mbarouk	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyiddin Moh'd Muhyiddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.

42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
59.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.

62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake.

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim      Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

## **Kikao cha Saba – Tarehe 30 Januari, 2009**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

### **DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

### **MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 87**

#### **Zanzibar kuitumia Wizara ya Mambo ya Nje ili kufaidika katika Muungano**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin** - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 102(1), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na mamlaka kamilii juu ya mambo yasiyokuwa ya Muungano kama yalivyoordheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba hiyo. Kwa kuwa mambo ya nchi za nje ni miiongoni mwa mambo ya Muungano.

- (a) Je, Mhe. Waziri, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaitumiaje wizara hii katika kutekeleza shughuli zake za kiutendaji hasa zile za kiuchumi ?
- (b) Kwa kuwa Sera ya Tanzania katika mambo ya nje ni kuimarisha uchumi wake kwa njia ya diplomasia. Je, Serikali ya Zanzibar inaitumia viipi fursa hii katika kuijiunga na Jumuia ya nchi za Kiislam (*OIC*) katika kuimarisha uchumi wake ambao unaonekana bado ni duni ?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kutuamsha siku hii ya leo tukiwa wazima kabisa wenye afya njema.

Baada ya hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa lengo la kutoa fursa sawa kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama zilivyo Taasisi nyengine za Muungano Ofisi ya Mambo ya Nje inayo ofisi yake hapa Zanzibar ambayo wajibu wake ni kuratibu shughuli zote zinazohusu mambo ya Nje Kiuchumi, Kisiasa na Kidiplomasia.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kutoa jibu kama hivi ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaitumia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufanikisha mambo kadhaa ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na safari za nchi za nje za viongozi wetu wakuu na viongozi wa Nchi za Nje wanaotembelea Zanzibar.

Mhe. Spika, mambo mengine ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ikinufaika ni kwa watendaji wakuu wa SMZ wakiwemo baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kushirikishwa katika baadhi ya ziara za nchi za nje za viongozi wakuu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniania. Pia viongozi watendaji wakuu wa SMZ walishirikishwa katika vikao nya mikutano ya Kimataifa.

Mhe. Spika, ni dhahiri Zanzibar imenufaika sana katika kujitangaza kwa wawekezaji na hasa katika Sekta ya Utalii na Ushirikiano kwa Nchi na Mashirika mbali mbali ya Misaada ya Kimataifa ambayo ni dhahiri maendeleo makubwa yamefikiwa kupitia misaada iliyopatikana kupitia kwao.

- (b) Mhe. Spika, kama nilivyowahi kujibu katika jibu Nambari 86 ni kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mgawanyo wa majukumu ya serikali zetu mbili suala la mambo ya nje ni suala la Muungano. Uanachama katika Mashirika mbali mbali ya Kimataifa likiwemo lile la Jumuia ya Nchi za Kiislam (*OIC*) ni suala la Mambo ya Nje ambapo Serikali ya Muungano ndiyo yenyenjumku la kuomba uanachama huo.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa suala la mambo ya nje ni suala la Muungano, lakini biashara na uchumi si suala la Muungano. Kwa kuwa sera ya nje ya Tanzania sasa hivi ni diplomasia ya kiuchumi. Je, Zanzibar ina nafasi gani katika ofisi za

mabalozi kuwa na mjambe wake maalum anayeshughulikia mambo ya kiuchumi na biashara kwa Zanzibar ?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba suala la mambo ya nje ni mambo ya Muungano lakini zaidi sasa hivi katika sera ya mambo ya nje tunaangalia suala la kiuchumi na diplomasia.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako nataka kulipa taarifa Baraza lako tukufu kwamba miongoni mwa vikao vyetu vya kero za Muungano suala hili alilolizungumza Mhe. Rashid Seif ni suala ambalo tunalifanya kazi. Hivi sasa kumetolewa kazi kwa Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje kuandaa utaratibu katika kila ofisi zetu za kibalozi basi ni lazima kuwe na mjambe ambaye atayekuwa anatokea upande wa Zanzibar. Hili wazo la kusema kwamba kuweka afisa ambaye atashughulikia masuala ya kiuchumi, Mhe. Spika, hili nitalichukua na katika hayo mapendekezo tutakayoyatoa baada ya huo muundo katika balozi zetu za nje basi tutahakikisha kwamba katika ofisi zetu za balozi za nje tutaweka watu ambao watakuwa na sifa hizo ambao watakuwa na majukumu ya kuweza kushughulikia mambo ya kiuchumi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba tupolee kidogo haya masuala kwa vile tunayashughulikia haya mawazo yenu ambayo mnayatoa yataweza kutusaidia katika kupendekeza wale maafisa ambao watawekwa katika balozi za nje wawe na sifa au wawe na kazi kama hizo alizozitaja Mhe. Rashid Seif.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Mkuregenzi wetu wa Mambo ya Nchi za Nje tumemuita rasmi hapa aje asikilize maoni ya waheshimiwa hasa katika hili maswali yatavyojitekeza. Kwa hivyo, naamini akiondoka hapa katika yale mapendekezo ya maafisa wa kibalozi watakaokwenda katika balozi zetu tofauti za nje basi moja katika kazi watakayopewa iwe ni masuala ya kuratibu mambo ya kiuchumi kwa Zanzibar. Ahsante.

**Mhe. Soud Yussuf Mgeni:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa makanisa yameshaikemea Serikali ya Jamhuri ya Muungano isijiunge na *OIC*, naamini haitajiunga. Kipi kinachozuia Zanzibar isijiunge moja kwa moja ?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, Mhe. Soud Yussuf maswali yake yana uchokozi uchokozi. Mhe. Spika, Taasisi za Kidini zina haki ya kuzungumza jambo lolote ambalo wanahisi kwamba na wao wanaweza kutoa maoni yao kama ni wananchi wa kawaida. Suala hili

la Zanzibar kujiunga na *OIC* hili limezungumzwa zaidi Bungeni. Makanisa lakini sio peke yao hata na wenyewe misikiti vile vile na wao walilizungumza sana. Kwa hivyo, malumbano yalikuwa baina ya makanisa na pamoja na misikiti, lakini bado chombo cha Bunge ni sawa sawa na Baraza la Wawakilishi, inapokwenda mijadala Bungeni pale zaidi wanaosikilizwa ni Wabunge sio watu waliokuweko nje.

Kwa sababu sasa hivi kuna demokrasia, kuna uhuru wa kutoa maoni, kuna uhuru wa kujielea hivyo kila mtu atatoa maoni yake tofauti kupitia kwenye magazeti au katika mihadhara yao mbali mbali. Kubwa zaidi Wabunge wenyewe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mionganoni mwao wamo Wabunge kutoka Zanzibar basi wao ndio wanaotakiwa kutoa maamuzi yale na bila kuangalia shindikizo la makanisa au jengine.

Mhe. Spika, lakini pia katika suala la Zanzibar nadhani msimamo wetu tumeshautoa kama ilivyoelezwa suala la kujiunga na Jumuia za Kimataifa ni suala la Muungano na Zanzibar ilipokuwa na mchakato wa kutaka kujiunga tukazuwiwa tukaambiwa tusibiri Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, ndio hivi sasa tangu lilikuwa linazungumzwa nje mpaka limeshafika Bungeni tunaamini liko katika hatua za mwisho na mapendekezo yetu Zanzibar kama itafika pahala Bunge la Jamhuri ya Muungano wataona bado kujiunga na hii jumuia basi Zanzibar rasmi kama tulivyosema tutaomba tujiunge sisi. Baada ya kuona mafanikio ya kiuchumi watayoyapata Zanzibar tunaamini na wenzetu wataingia shauku nao kuwa na hamu ya kuendelea na kujiunga na jumuiya hii.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Suala la *OIC* Zanzibar ilikuwa imeshakubaliwa kuwemo na Jamhuri ya Muungano ikatutaka tutoke. Hilo Mhe. Waziri analijua?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, ni kweli najua kwamba Zanzibar ilikuwa imeshakubaliwa kujiunga na Jumuia hii ya *OIC*, ndio maana baada ya kuona tumeshakubaliwa wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakaona kwa mujibu wa katiba kidogo tumekiuka na ndio maana wakatwambia tusimame kwanza tusubiri tuingie sote. Kama nilivyosema mwanzo kuwa suala hili ni la muda mrefu, lilikuwa linazungumzwa juu juu na hivi sasa linazungumzwa ndani ya Bunge na kwenye Bunge ndipo panapopitishwa maamuzi makubwa hasa yanayoambatana na katiba.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba tunategemea kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Nchi za Nje baada ya utafiti wa muda mrefu imeonekana kwamba Jumuia ya Nchi za Kiislamu haiathiri mambo au utamaduni wa nchi yoyote ikiwa ya Kikiristo au ya Kiisilamu kwa sababu jumuia hii zaidi imejikita katika mambo ya kiuchumi. Bado tunategemea kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itajunga katika jumuia hii kwa maslahi ya Watanzania wote bila ya kujali tabaka kama Wakristo au Waislamu au Wapagani. Kwa hivyo, tunategemea kwamba Jamhuri ya Muungano itajunga.

Vile vile kama nilivyosema mwanzo kama wataona wao bado kujiunga basi tutaomba rasmi kupata kibali kujiunga zaidi katika masuala ya kiuchumi. Ahsante sana Mhe. Spika.

### Nam. 108

#### Taa za Barabarani (*Street Lights*)

**Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-**

Pamoja na kuweka haiba ya mji, taa za barabarani ni muhimu kwa usalama. Kwa kuwa taa hizo zimeharibika kabisa katika barabara nyingi na kwa kuwa baadhi ya barabara hazina kabisa taa hizo.

Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuzifufua taa zilizoharibika na kuweka taa kwenye barabara ambazo hamna taa kabisa?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali inalieleta sana tatizo sugu la taa za barabarani. Ili kuliondoa tatizo hilo, serikali imeshafanya mazungumzo na Benki ya Dunia na tayari benki hiyo imetenga Dola za Kimarekani 3,000,000 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo taa za barabarani za Mjini. Kwa kuwa mradi huo haujaaanza, hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni kuzihamasisha kampuni zinazoweka mabango ya matangazo njiani kuzifanyia matengenezo taa za barabarani. Kwa kuanzia kampuni hizo zimeanza na barabara ya Salmin Amour na barabara ya Nyerere na hivi sasa taa hizo zinawaka. Tunategemea kampuni nyengine zitaanzia Kilimani kuititia kariakoo hadi Kisiwandui.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nakubaliana na Mhe. Waziri katika maelezo yake mazuri labda pana wafadhili kuwa Benki ya Dunia iko tayari kuhakikisha taa zote za njia zetu za Zanzibar zinawaka. Lakini kwa kuwa ni muda mrefu taa hizo bado zipo katika maeneo ambayo maguzo yamo lakini taa haziwaki. Tumeshuhudia kwa macho yetu baadhi ya waheshimiwa wote waliokuwemo humu na wananchi kwa jumla hivi sasa kuna ukarabati wa utajji rangi maguzo hayo. Je, hao watu wenye kuweka mabango ya biashara wanaona lipi la muhimu kulifanya kati ya kutia rangi na kuweka taa zikawaka kwa muda kabla ya huo mpango mkubwa haujafika?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, suala la taa za njiani ni kero kubwa kwa sababu mji ukikosa taa za kumurika mji unakuwa si mzuri na halafu usalama unakuwa mdogo sana. Lakini hata hivyo, juhudhi tulizozichukua ni hizo na hao wawekezaji wengine ambaao wanapenda kuweka mabango yao ya barabarani kutangaza biashara zao pia tumewashawishi kufanya usafi katika maguzo hayo na kuzikarakabati taa hizo. Hata hivyo, ikiwa Mhe. Ali Suleiman una ushauri wowote zaidi ya huu tutapendelea kuuchukua ili tuweze kuufanyia kazi.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kujibu swali la msingi na la nyongeza. Lakini hata hivyo napenda kumuuliza swali moja la nyongeza lenye a na b.

- (a) Mhe. Spika, kwanza ningependa kujua, huu mpango ambaao tunategemea kusaidiwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia utajumuisha miji mingapi katika visiwa vyetu vya Zanzibar?
- (b) Mhe. Spika, hivi sasa Baraza la Manispaa lina mradi wa kupaka rangi nguzo zote za umeme katika Mji wa Unguja nguzo ambazo haziwaki. Je, Mhe. Waziri mradi huu unafanywa kwa maslahi gani na utagharimu kiasi gani?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, kweli tunazungumzia ni miji mikuu ya visiwa vyetu ndio itawagusa kutokana na mpango huu ambaao tunatarajia kupata msaada kutoka sehemu nyengine.

Suala la kupaka rangi nguzo kwa kweli siwezi kusema zitagharimia sehemu gani, lakini kwa wale wote ambaao wanaendelea kuweka mabango yao ni kutia rangi pamoja na maguzo ambayo yapo. Kuhusiana na suala hili baadhi ya nchi ambazo zimeendelea wana utaratibu wa kupaka rangi nyumba zile zote ambazo ziko katika *main road* kila baada ya miaka mitatu na wengine

minne. Sisi labda tutaanza na maguzo ili tuweke usafi mzuri pamoja na nyumba zinazohusiana. (*Kicheko*)

### Nam. 103

#### Vitendea kazi katika Usafi wa Barabara

##### Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa na wananchi wetu ni uchafu wa barabara zetu za Mjini ambazo mbali na uchafu lakini pia zimejaa michanga, hali ambayo pia huchangia ajali za barabarani.

- (a) Je, Mhe. Waziri, ni lini wizara yako italishughulikia ipasavyo tatizo hili?
- (b) Wasafishaji wa barabara hizi hutumia mapauwo na zana nyengine duni. Je, Mhe. Waziri, wizara ina tatizo lipi linalokwamisha kuwa na vitendea kazi bora ?

##### Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 103 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Ili kulishughulikia tatizo la kujaa michanga katika barabara za Mjini, linahitajika gari maalum la kisasa kwa kazi hiyo au kuajiri wafanyakazi zaidi ya tuliokuwanao. Lakini kwa sasa Baraza la Manispaa halina uwezo wa kuyafanya yote hayo mawili. Hali ya fedha itakaporuhusu tatizo hilo litashughulikiwa ipasavyo.
- (b) Tatizo linalokwamisha kuwa na vitendea kazi bora kwa ajili ya usafishaji wa barabara ni ukosefu wa fedha, kwani gharama ya gari la kusafishia pamoja na vifaa vya kufyagilia si chini ya Dola za kimarekani 105,000 sawa na Tshs. 135,000,000/= ambazo kwa sasa Manispaa haina uweo.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Nafikiri suala kubwa lililozungumzwa hapa juu ya matatizo ambayo yanajitokeza katika barabara zetu za Manispaa ya Zanzibar. Kwa kweli barabara hizo

wafanyakazi au wananchi wanajitahidi kusafisha lakini kutokana na wingi wa mchanga au uchache wa wafanyakazi huleta usumbufu mkubwa.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa kuna matrekta madogo tena bei nafuu sana na kama litakuweko moja tu katika mji wetu wa Unguja na likizunguka kutwa litafanya kazi nzuri ili kuondoa usumbufu na kupunguza kuajiri hao wanaotakiwa kuajiriwa ili wasafishe maeneo hayo. Wizara ina mpango gani? Na kama Mhe. Waziri atakuwa tayari nimpeleke yanapouzwa ili ayapate kwa bei nafuu si kiwango alichokitaja yeye hicho ni kiwango cha chini kabisa je, anasemaje?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, kwa ninavyojuua mimi matrekta hutumika kwa kulimia. Sasa nashindwa kulijibu swali hili kuyatia matrekta katika barabara. (*Kicheko*)  
Mhe. Spika, hata hivyo, nilichozungumzia mimi ni kwamba kuna gari maalum linatumika katika kuzoa mchanga katika barabara na gari hilo ndilo lenye uwezo mkubwa kabisa na ndio wenzetu wanilotumia na nikataja bei ya gari la aina hiyo kwamba karibu shilingi 135 milioni ambazo kwa sasa si rahisi kuzipata kwa kuziingiza katika mradi huo. Lakini hata hivyo, hilo suala la matrekta Mhe. Ali Suleiman tukutane halafu utueleze ni matrekta ya aina gani hayo ili serikali iweze kuyaagiza kama bei itakuwa ni nafuu.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsanet sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri mimi namuuliza kwamba pamoja na hayo majibu yake lakini hakuna ndogo ya gari kama hiyo? Kwa sababu tukitembea katika nchi nyengine utakuta liko kubwa na viko vidogo vidogo na sisi ni kisiwa, basi katika hayo ya kusafishia mchanga hakuna vidogo vidogo ambavyo tunaweza kuvimudu wamefanya utafiti?

Pili hata kabla ya hiyo gari ni utaratibu gani unaotumiwa na Manispaa kusafisha angalau kila wiki barabara moja?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, ushauri wake kuhusiana na hizo gari ndogo zipo, lakini kwa urahisi kuna gari maalum ambalo linaweza ku-cover maeneo makubwa kwa muda mchache ambalo hili ndilo tulilolilenga sisi. Kuwa na vigari vidogo vidogo ambavyo vinashughulikia kuweka usafi wa mji suala hilo tumehisi itakuwa ni gharama kubwa kuliko kuwa na gari moja ambalo linaweza kuchukua masafa marefu, muda wake wa kufanya kazi ni mrefu, lakini hivi vigari vidogo vidogo bado itabidi tuongeze ajira kwa kushughulikia vigari hivyo ambavyo Rashid Seif ametushauri.

Hata hivyo, kama nilivyozungumza kwa Mhe. Ali Suleiman ni suala ambalo bado linahitaji utafiti wa kina kwa sababu barabara zetu zilivyo mchanga na barabara hauko mbali. Kutokana na hali hiyo ndio maana tukakuta mchanga unakuwa mwingi kwenye barabara *almost* sehemu kubwa ya mji wetu. Kwa hivyo, katika kushughulikia usafi huo ndio maana baadhi ya taasisi huwa tunawajaribu au maskani ili kushughulikia kusafisha maeneo mbali mbali. Kwa mfano, walianza kule Kwahani sehemu kubwa ambayo ilikuwa ina michanga katika barabara wameweza kusafisha, sehemu ya Amani, kwa hivyo, vikundi hivi bado tuvihamasishe ili kuweza kuweka mji wetu safi na salama.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii kutoa maelezo ya ziada pale alipomalizia Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Nionavyo mimi suala la usafi wa barabara na maeneo mengine ya nchi yetu yanategemea mambo mawili. La kwanza kuwa makini kusafisha hizo barabara kwa kutumia mifagio katika hali yetu ya umasikini tuliyonayo na hili kwangu mimi kwa nchi masikini kama yetu naliona ni jambo la msingi sana. Kwa sababu hizo fedha zenyewe za kutafuta hayo magari madogo na makubwa pengine sasa hivi hatunazo, lakini mimi naamini uwezo kama tutakuwa makini wa kufanya hii kazi Baraza la Manispaa wanao.

Kuna kipindi kama mwezi mmoja, miwili au mitatu tulifanya zoezi maalum chini ya usimamizi wa Waziri Kiongozi. Kwa hivyo, naliagiza Baraza la Manispaa kabla ya kutafuta hizo fedha kwa ajili ya kununua magari madogo na makubwa kwa ajili ya kusafisha mchanga barabarani waanze na zoezi maalum angalau kila wiki mara moja. Kwa sababu huu mchanga ni kweli barabara zetu chini sana katika baadhi ya maeneo na inakuwa rahisi sana kukaa mchanga, lakini angalau tukifanya hiyo kazi angalau wiki mara moja au mbili hali haitakuwa kama hivi ilivyo, wakati mwengine wanachukua muda mrefu sana na Afisi ya Waziri Kiongozi baada ya kumaliza Baraza hili tukufu, pengine katika kipindi kimoja ama viwili hivi kama tulivyosimamia zoezi la kufanya usafi katika maeneo ya mijini tutafanya zoezi maalumu. Pengine umefika wakati na namuagiza Mhe. Waziri katika Afisi wa Waziri Kiongozi. Mhe. Waziri wiki ijao wakusanye wafanyakazi wote wa Baraza la Manispaa na pengine tuwasimamie mimi na wewe wagaiwe kazi maana pengine inaonekana labda utaratibu wa kugawa hizi kazi unaonekana mgumu.

Naamini tukifanya hivyo halafu baadaye tuwaelekeze wengine namna ya kusimamia wafanyakazi wao angalau inawezekana kazi hizi zikafanywa. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*).

## Nam. 94

### Msongamano wa Magari Bandarini

#### Mhe. Salmin Awadh Salmin– Aliuliza:-

Tatizo la msongamano wa magari pamoja na abiria katika Bandari ya Malindi sehemu ya abiria linaonekana bado linaendelea na kusababisha hatari kwa wananchi na usumbufu mkubwa. Kwa kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe, tayari imeshatoa kibali kwa ajili ya kujenga Jengo la abiria na kutengeneza sehemu ya maegesho ya magari. Na kwa kuwa Taasisi zinazotumia eneo hilo tayari zimeshahama.

- (a) Je, Mhe. Waziri ni lini kazi za ujenzi huo zinatarajiwu kuanza ?
- (b) Huo ujenzi wa Jengo la abiria utahusisha pamoja na sehemu ya viongozi mashuhuri (*V.I.P*) .?
- (c) Mhe. Waziri, utakubaliana nami kuwa wanaosimamisha magari yanayoingia bandarini maeneo ya “round about”, wanaleta usumbufu mkubwa kwa magari mengine yanayotaka kuingia bandarini.

#### Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, ninaomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake nambari 94 lenye vifungu a,b, na c kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, mradi wa ujenzi wa Jengo la Abiria katika bandari ya Malindi uliana mwaka 2008 na unaendelea na umeingizwa katika bajeti ya kazi za Maendeleo za Shirika la Bandari kwa mwaka 2009. Matayarisho ya ujenzi huo tayari yalikwishaanza kwa kutayarisha michoro na makisio na kazi ya ujenzi inategemewa kuanza muda wowote kutegemea hali ya fedha ya Shirika.

Hivi sasa Shirika la Bandari likishirikiana na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (*UUB*) ili kujenga sakafu za lami katika eneo lililovunjwa banda lililokuwa likitumiwa na Idara ya Leseni kwa ajili ya kutengeneza maegesho ya magari ambapo, ambapo *UUB* mwishoni mwa mwezi wa Disemba, 2008 waliwasilisha makisio ya ujenzi huo na

Shirika linaendelea kuyafanya kazi. Ujenzi wa maeneo ya maegesho utaanza mara tu taratibu za ujenzi zitakapokamilika.

- b) Jengo hilo la abiria litakuwa na sehemu maalum ya kufikia wageni mashuhuri (*VIP*).
- c) Nakubaliana na Mheshimiwa kuwa kusimamisha magari katika eneo la “*round about*” ya kuingilia bandarini unaleta usumbufu kwa watu wengine, lakini huo ni utaratibu wa Jeshi la Polisi ambao unakidhi haja ile ya kutokuwepo kwa msongamano yaani bila ya hapo msongamano ungekuwa mkubwa zaidi. Lakini hata hivyo wizara yangu itakaa na Jeshi la Polisi ili kupunguza msongamano huo wa magari katika eneo hilo.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

- (a) Mhe. Spika, ni lini kwa mujibu wa *plan* iliyaondaliwa kazi hii itamaliza na usumbufu huu utaondoka.
- (b) Ile sehemu kuna kipindi cha nyuma kidogo tu hivi kulikuwa na vikuta vimepangwa kati kati ya barabara na sasa hivi nimepita jana vikuta havipo tena ni kitu gani kilichofanywa viwekwe vikuta na kitu gani kilichofanywa viondolewe vikuta vile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:**

- (a) Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika suala la msingi ni kwamba kukamilika kwa ujenzi huu kutategemea zaidi na upatikanaji wa fedha. Lakini nia yetu ni kujenga na kumaliza kwa wakati mzuri.
- (b) Ni kweli kuliwekwa vikuta na sasa hivi havipo, viliwekwa kwa kuzuia magari yasiende kule yaani yawe yanapita sehemu moja tu. Lakini hata kufunguliwa kwake sasa hivi kumewezesha baadhi ya magari yaende katika eneo lile pale kabla ya kuteleta msongamano. Zipo gari zinaishia pale na zinarudi pale pale.

**Nam. 109**

**Maandalizi kwa Ajili ya Uchimbaji wa Mafuta**

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Aliuliza:

- (a) Mhe. Waziri, wizara yako imefanya utaratibu gani wa kuwaandaa vijana wetu kuchukua nafasi za ajira wakati utakapofika wa kuchimbwa mafuta ambayo inasemekana yapo Zanzibar na itakapofikiwa mwafaka juu ya namna bora ya kulishughulikia suala hilo baina ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ?
- (b) Kwa kuwa uchimbaji wa mafuta hufuatana na uchafuzi wa mazingira, serikali imeandaa mkakati gani kukabiliana na hali hiyo wakati wa uchumbaji wa mafuta hayo ukifika ?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati wa Ardhi - Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 109 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

- (a) Mhe. Spika, suala hili linafanana na suala Nam. 14 lakini kwa faida ya Mhe. Mwakilishi napenda kumhakikishia kuwa wizara yangu inayo mikakati madhubuti ya kusomesha vijana wetu kwa kuwapeleka katika vyuo mbali mbali ndani ya nje ya Tanzania. ?

Mhe. Spika, kwa kawaida Makampuni yote ya utafutaji wa mafuta katika mikataba yao kipo kipengele cha mafunzo *Training Programme* kwa mfano mikataba wa uliozuiliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzinbar mwaka 1997 ulikuwa na kipengele cha Dolla za kimarekani *50,000* kwa mwaka kwa mafunzo na kuna baadhi ya Makampuni ambayo yamekubaliana na *TBDC* wao wana vipengele vya Dolla za kimarekani *100,000* kwa mwaka kwa ajili ya mafunzo.

Mhe. Spika, ikiwa tutardhia utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi asilia hapa kwetu basi kwenye mikataba hiyo nayo kutakuwa na vipengele maalum kwa ajili ya mafunzo, na hiyo itawezesha kuwasomesha kwa kasi zaidi Wazanzibari ili kuitumikia nchi yao kwenye sekta hii.

Mhe. Spika, katika mikataba hiyo nayo suala la mazingira hupewa umuhimu wake ikiwa kampuni yenye kutafiti kuchimba mafuta itaharibu mazingira itapaswa kutoa fidia kwa uharibifu huo.

Mhe. Spika, hata hivyo kampuni huwa hazipaswi kulipia uharibifu wa mazingira peke yake. Lakini pia inatakiwa kulipa uharibifu wa mazao uhamishaji wa watu katika maeneo yao ya asili, uharibifu wa miundo mbinu nakadhalika.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na kusubiri mengineyo ambayo tunatafuta moja au mbili ikubalike ili watu hao waanze kufanya kazi hizo za mafunzo. Je, kwa kuwa mtiririko mzima unaendelea huku katika kuutafuta huu mwafaka wenyewe na tunaamini muafaka huo kwa asilimia mia moja utakuwa kwa Wazanzibari.

Je, serikali wenyewe kwa upande wetu inaandaa vipi vijana wetu hao kutafuta japo huduma za mwanzo tu ya kuanzia ili wajihakikishe kwamba wanajiweka tayari.?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati wa Ardhi:** Mhe. Spika, niombe niweke jambo moja sawa kwa maoni yangu mimi.

Kweli tumo kwenye mtiririko lakini alitumia maneno tukifika pahali kuomba. Mimi sidhani Zanzibar inaomba. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar imengia katika Muungano ikiwa nchi Huru na Zanzibar ina mamlaka yake kamili. Tukiwa ndani ya Muungano tuna wajibu wa kushauriana kwa yale yaliyotuhusu sio kuomba hatuombi kwa maana hatutawaliwi na mtu.

Pia kama nilivyoeleza katika kikao hiki hiki kwamba Baraza la Mapinduzi likifika kufanya maamuzi yake maamuzi yanayohusiana na suala hili yataletwa kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa maamuzi kwa niaba ya Wazanzibari na baada ya hapo serikali itaendelea kukata mashauri na kulielekeza suala hili.

Pia nilieleza kwamba tayari tuna mazungumzo na Serikali ya Norway kupitia shirika lake la *Oil for Development* tayari wameshakuja kufanya tafiti za awali kuelewa nini tunahitaji na wapi au katika fani ipi tunahitaji kuwa na vijana ambao wataweza baadaye waanze kuandaliwa ili waweze kusaidia nchi yao. Hivi sasa tunasubiri hatua za mwisho na maamuzi ya mwisho ya Serikali hiyo ya Norway.

**Mhe. Aziza Nabahan Suleiman:** Mhe. Spika, leo asubuhi nilipokuwa nikisikiliza Vyombo vyta Habari nilisikia *Redio One* ikisema maneno kuhusu mafuta na mtangazaji Farouk Karim alisema kwamba tayari muelekezi ameshatoa taarifa kwamba Zanzibar hatuna mafuta ya biashara lakini tuna mafuta kama ya matumizi tu. Kwa hivyo, je tunaendelea na

ushauri wa mwelekezi mwenye kutuambia hatuna mafuta Zanzibar au tunatafuta mwengine.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati wa Ardhi:** Mhe. Spika, tulipokuwa na semina ya Mshauri mwelekezi pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote tulifika pahali tukamshutumu yule bwana kuwa pengine sasa ameshalainishwa na anatizama maslahi ya upande mmoja. Lakini hivyo hivyo tulikubaliana hata ikiwa ni "Nibu" tutajipaka wenyewe.

Lakini maamuzi ambayo mimi nyaamini ambayo yatafanywa na Baraza hili la Wawakilishi yatalenga zaidi kutizama mustakabali wa wananchi wa Zanzibar na vizazi vetu vijavyo na heshima ya nchi yetu. Kwa hivyo, kama kuna "Nibu" kama nilivyosema wenyewe. Mkiamua kwamba hiyo "Nibu" tutajipaka wenyewe na Gesi mtanusa mtaamua wenyewe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu wake mazuri sana na pili nampongeza pia kwa kutuletea ile semina ya awali hapa ndani ya Baraza ambayo ilituelimisha sana kuhusiana na masuala haya ya mafuta na naamini ameshaahidi kwamba itakuja nyengine hiyo ripoti itakapokamilika.

Mhe. Spika, Mhe. Malima kule Tanzania Bara juzi katika Bunge alizungumza kwamba Zanzibar hakuna mafuta. Lakini wakati huo huo hawa hawa *TPDC* kuna mkataba ambao tayari wameshausaini na Kampuni kubwa ya nje ambayo inaitwa *Antrim* kuwa hivi vitalu vyta hapa Zanzibar na mkataba huo ni mkubwa na ni wa mamilioni ya fedha. Sasa je, Mhe. Waziri anatuambia nini, kule Mhe. Waziri anasema hakuna mafuta lakini mamlaka yake kuu ya mafuta tayari imeshatiliana mktabata na ule mkataba umezuiila na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mpaka hapo maafikiano yatakapofikia. Sasa Mhe. Waziri anatueleza nini kuhusu hili ?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati wa Ardhi:** Mhe. Spika, kwanza naamini kwa hali hii na muamko uliokuwemo mionganoni mwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba waraka ule wa maamuzi ya serikali utakapoletwa kwenye Baraza hili tukufu kwenye kikao chake hiki kinachofata ikiwa Machi au Aprili patakuwa na mjadala mzuri sana na nisisitize kwamba kama nilivyowashauri Wajumbe wa Baraza hili tukufu wajiandae kwa maana kitakachosaidia Wazanzibari kufahamu suala hili ni misingi ya hoja ili walimwengu watufahamu vizuri zaidi ni msingi wake utakuwa ni hoja tena za kina na hata mjadala wetu mionganoni mwa pande zote mbili hizi za Muungano bado tutaendelea kuwa na misingi ya hoja.

Kulikuwa na moja siku ile nilisahau niwashauri pia Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuwa waitafute sheria hiyo. Sheria hiyo ni sheria Nam. 15 ya mwaka 1984 inaitwa "Sheria ya Umoja wa Mataifa" mkiingia kwenye Mtandao wa Umoja wa Mataifa sheria hiyo mtaipata kwa sababu ushauri ule wa mwelekezi pia unazungumzia namna ya kugawana maeneo ya Bahari Kuu.

Kama tunavyoolewa Katiba ya Zanzibari inatupa fursa ya *Exclusive Economic Zone*. Kama tunavyoolewa Katiba ya Zanzibar inatupa fursa ya *12 nautical miles* ndio maeneo ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar hapo ndipo kwenye mamlaka yetu.

Baada ya hapo yanaingia sasa mamlaka ya pamoja kwa maana ya Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania. Kwa maana hiyo ni vyema sheria hiyo nayo Wajumbe wakaipata na wizara ikafanya jitihada nayo.

Jengine nilisahau kwamba katika mchango wa Mhe. Ali Mzee Mwenyekiti wa Baraza hili wakati tunachangia Bajeti na kwenye semina ile. Kwa kweli alitoa mtiririko mzuri wa historia ya utafutaji wa mafuta katika nchi yetu alitoa mpangilio mzuri tu unaohusiana na masuala yanayohusiana na masuala ya Muungano pamoja na sheria zinazotawala Muungano wetu na mengineyo.

Kwa hivyo, nalo hilo pamoja na mengine tuliyoyasema Wawakilishi wayapate ni muhimu yafanyike.

Nikijibu suala la Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, niweze kudokeza kidogo, tu hata mshauri mwelekezi katika ushauri wake amekubaliana na jambo moja la msingi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa sahihi kuzuia mkataba ule kutokana na utata uliokuwepo kwa kisheria na wa kikatiba, na hilo litabainika ziadi tutakapoyazungumza haya masuala na nilisema wapo Wawakilishi wengi humu ndani wenye usoefu mkubwa sana na upeo mkubwa sana, wako kwa upande wa Chama cha Upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Soud Yusuf Mgeni na wengineo na wapo wengi sana kwa upande wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Ali Juma Shamhuna na wengine pamoja na wewe Mhe. Spika. Nategemea kwamba tutaweza kupata katika huo usoefu wao na wengine kujifunza na pengine kuelekeza maamuzi yetu.

Mhe. Spika, niweze kusisitiza tu kwamba halina Teknolojia ya mia juu ya mia inayoweza kusema kuwa pahali yapo mafuta, unaweza kupata mwelekeo kutokana na tafiti za mtetemo.

Zanzibar yetu mwelekeo kwa tafiti na taarifa zote tuliokuwa nazo kwamba mwelekeo wa kupata mafuta ni mkubwa. Tutatambua hapo watu watakapoanza kuchimba na kutafuta kuna kiwango gani, mafuta ya aina gani na yako ya namna ipi.

Mfano Mhe. Spika, hapa kwenye maji kuna wataalamu wanasema kuwa maji yanakuja juu kama chemchem wenyewe mafuta halikadhalika kuna maeneo mengine ndani ya dunia hii si maeneo mengi sana mafuta yanakuja juu wenyewe, pale Tundaua mafuta yanakuja juu wenyewe nafikiri na hii Tundaua iko kwenye jimbo la Mhe. Abdalla Juma.

Sasa kwa mnasaba huo mimi nafikiri hatimaye "Nibu, ndoo, geloni" yatakuwa maamuzi ya Wazanzibari wenyewe juu ya namna ya kuelekeza suala hili, yapo tutamshukuru Mwenyezi Mungu na hapo pia tutamshukuru. La kuomba kwamba Mwenyezi Mungu atujaalie neema hiyo itufae sisi na vizazi vyetu bila ya sisi kupigana na kugombana na iwe ni neema kwetu.

Sasa naomba tusibabaike na maneno tusubiri wakati wa kufanya maamuzi. Mhe. Spika nakushukuru.

## Nam. 105

### **Wananchi Kulipia Huduma ya Maji**

#### **Mhe. Ame Ussi Juma - Aliuliza:**

Pamoja na kuitisha Sheria inayoruhusu kuwepo kwa mfumo wa kulipia maji Zanzibar, inaonekana wazi kwamba, matayarisho ya utekelezaji wake hayajawa mazuri.

- (a) Je, Mhe. Waziri, hivi ni busara kuwalipisha wananchi huduma ya maji hali ya kwamba maji hayo hayatoki majumbani mwao ?
- (b) Kwa kuzingatia hali duni ya maisha ya wananchi wetu wa Zanzibar, Je, wizara imetumia vigezo vipi vya kuwatoza Tsh. 4000/- bila ya kujali kupatikana maji hayo majumbani mwa wananchi hawa ?

#### **Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:**

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza lako Tukufu la Wawakilishi imepitisha Sheria ya Maji Namba 4 ya mwaka 2006. Sambamba na hilo wizara yangu nayo ikapitisha Kanuni za Maji mwaka 2007 zilizofanyiwa marekebisho mwezi Agosti mwaka 2008 ili kupata uwezo Mamlaka ya kukusanya michango ya maji kwa wananchi.

Mhe. Spika, aidha katika kuendeleza maandalizi hayo na yale mengine ya kiutawala kama kufanyika kwa sensa ya kuwatambuwa watumiaji wa huduma ya maji kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi sensa ambayo itaendelea kwa Mikoa yote ya Zanzibar, uwekaji wa mtandao wa kutunza taarifa za watumiaji (*Customers Database*) pamoja na kukamilisha muundo wa utendaji wa Mamlaka ni sehemu ya juhudi za wizara za kufanya sheria hiyo itekelezeke ipasavyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache naomba kuendelea kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, katika hali ya kawaida maji kama ni huduma inatakiwa alipishwe yule anayoipata tu. Lakini katika hali ya sasa ya Zanzibar kuna changamoto kubwa inayokabili wizara yangu juu ya kuainisha kwa kina nani anapata huduma hiyo na nani hapati. Hii inatokana na ukweli kwamba watumiaji wote wa maji majumbani hawajafungiwa mita, hivyo inapelekea kuwe na utata wa wanaopata na wasiopata wote kuwa kwenye kundi moja, ndio maana Mamlaka ikasambaza bili kwa nyumba zote za Mkoa Mjini Magharibi ili kutumia fursa hiyo kufanya uchambuzi wa kina juu ya suala hilo.

Mhe. Spika, vile vile Sera ya Maji ya Zanzibar ambayo iliyopitishwa na serikali kupitia Baraza lako Tukufu imeeleza kwa kina juu ya vigezo vya kutathmini nani ameshafikiwa na huduma na nani bado, Sera hii inasema kuwa serikali itafahamu kuwa imeshawahudumia wananchi endapo watakuwa na uwezo wa kupata huduma hiyo si zaidi ya umbali wa mita 250 kwa Vijijini na mita 150 kwa Mijini.

Mhe. Spika, hata hivyo kwa nia ya kutowakandamiza wananchi, wizara yangu imetowa taarifa kuwa "*asiyepata maji asilipe*".

- (b) Mhe. Spika, sekta za huduma kama maji ulimwenguni kote zinapotaka kuweka viwango vya malipo zinatakiwa kuzingatiwa mambo makuu mawili nayo ni kuweza kurejesha gharama za

uendeshaji pamoja na kurejesha gharama za uchakavu wa miundo mbinu.

Kutokana na hali ya uwezo wa wananchi wa Zanzibar pamoja na ugeni wa kuchangia huduma hii kwa muda mrefu wizara ilizingatia zaidi mambo hayo (*ability to pay*), kwa kuchukua tathmini ya sensa ya kipato cha majumbani (House hold Budget Survey) ya 2005 inayofanywa kupitia Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, taarifa ambazo kwa mujibu wa kipato cha mtu wa kawaida kwa mwezi kina uwezo wa kulipa TZS. 3,750 kwa huduma ya maji tu. Vile vile kwa mujibu wa kima cha chini cha mshahara wa mfanyakazi wa serikali si zaidi ya asilimia 5 ya kipato cha mwezi ndio kinaweza kulipia huduma hii ambazo ni TZS. 4,000/=, hivyo wizara yangu ilifikia kutoza fedha hizo chini ya misingi niliyoitaja.

Baada ya kupitia tathmini hizi mbili pamoja na kujua kuwa Mamlaka itachukua muda mrefu zaidi wa kujiendesha wizara yangu iliona ni busara kuangalia zaidi uwezo wa wananchi wa kulipa na si vyenginevyo.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri kama kawaida majibu yake yanakuwa si ya ubabaishaji yanakuwa ni ya kweli haswa.

Pamoja na hivyo mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa kama ifutavayo:-

- (a) Kwa kuwa wakati tulipokuwa tukijadili Mswada wa Sheria ya Maji mswada huu ulikuwa majadiliano makali. Alisema kwamba Mheshimiwa kuwa asiyepata maji alisilipe mpaka kwa uhakika. Lakini kwa mchango wangu mkubwa kabla ya maji kupatikana saa 24 bado. Je, Mheshimiwa wakati utendaji wako watakapotayarisha huu utaratibu wa maji hawakuangalia *hansard* za Baraza wakaona hii ahadi tulivoitoa kwenyalo Baraza lako tukufu ?
- (b) Suala inalitizama vipi suala la kuwa na mita kwa sababu mimi naona suala la kuwa na mita ndio litakalombana yule aliyetumia na ndio litakalomuokoa yule asiyetumia. Je, suala hili hasa mnalitazama vipi Mhe. Spika ?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, kabla sijajibu masuali yake mawili ninaona nirejee.

- (a) Wakati umefika sasa tukiwa nchi ya Visiwa Wazanzibari wenyewe sasa kuchukua dhamana yao ya leo na huko tuendako.

Mhe. Spika, dalili ziko wazi mfano kiwango ambacho maji safi yanafaa kutumika na wanaadamu yanapokuwa na *conductivity* *1200* tunayahisi maji chumvi midomoni wanadamu hali ya hivi sasa hasa katika maeneo ya nchi yetu Unguja na baadhi ya maeneo hasa Michamvi kuingia kwa maji ya chumvi inaongezeka siku hadi siku.

Maeneo ya rasilimali ya maji na vianzio vyta maji kwa bahati mbaya yanavamiwa na watu kama si Wazanzibari kwa maana wamekuja wafuje waondoke. Hali ni mbaya kuna visiwa kadhaa duniani vikubwa kushinda sisi kwa kweli wameshaanza kupotelewa na maji safi na salama.

Ikiwa wenyewe sisi Wazanzibari hatutofika pahali tukakubali dhamana ya kuendewa kwa maji sisi tuliokuwepo leo na hawa ambao tutawaachia nchi hii basi ndani ya miaka 25 hadi 30 tutakuwa na barabara nzuri umeme, majumba na faghari na mengine. Lakini hatuna na nchi tutaihama. Mhe. Spika, Singapore hali hiyo sasa ya maji inaelekea huko.

- (c) Mhe. Katika kuelekea au kufikia malengo ya nchi yetu ya *vision 2020* tunahitaji karibu ya bilioni 450 kwa maji masafi na maji machafu kuelekea viwangi vile ambavyo tunavihitaji.

Hakuna mshiriki wa maendeleo hata kabla ya hali ya uchumi wa dunia kuanza kuharibika, walituambia kinaga ubaga kwamba kama hamtowezesha kuchukua jukumu na dhamana nyinyi wenyewe angalau basi kuchangia huduma ya maji pesa zetu hamtoziona na waliunganisha maji na umeme kwa sababu asilimia zaidi ya 98 ya vianzio vyetu vyote vyta maji Unguja na Pemba, hata vile vinavyopeleka Tumbatu, basi vyote vinategemea umeme kwa maana ya visima virefu, vianzio kwa maana *natural wells* ni kidogo sana. Kwa Shariff Ali pale Pemba na maeneo mengine mawili Pemba nafiriki Mwanyanya na Bububu takriban kwa asilimia kubwa sasa imeshaanza kupotea.

Kwa hivyo, alituambia kama hamtarekebisha sera yenu ya maji, basi fedha za Pemba tusingezipata za kupeleka umeme Tanga hadi Pemba. Hata huu mradi wa *MCC* unaotoka Ras Kiromoni kuja Fumba waya wa pili, basi

fedha tusingezipata. Hili lilikuwa jambo la msingi na wazi, serikali isingeweza kukataa na nyinyi wenyewe baada ya kulizungumza hili ndani ya Baraza la Wawakilishi mlikubaliana na hayo. Kwa hivyo, nilitaka nitoe tu utangulizi huo.

Nikiendelea Mhe. Spika, ni sahihi kwamba wizara yangu ilitoa ahadi kuwa wananchi tutawatoza michango pale ambapo watakuwa wanapata maji ya uhakika, tukatoa na vigezo. Ni kweli kwa asilimia kubwa hilo tumeshindwa kulifanikisha. Lakini hivi karibuni tu, nilikuwa na kikao na Wajumbe wa Bodi wa Mamlaka ya Maji na Menejimenti yake. Niliwataka wafanye mapitio upya kutizama kiwango hiki cha Shs. 4,000/- yale malengo tuliyojiweka kama hatujaweza kuyafikia au tumeyafikia.

Pili, wafanye zoezi maalum la kupita kwenye kila Shehia na kuzungumza na wananchi juu ya kwanini tumefanya hayo tuliyoyafanya na kuzidi kupata maoni yao. Mhe. Spika, haimaanishi kwamba serikali inavyofanya maamuzi haiwezi kujirudi. Serikali ni ya watu, na watu wanapofika pahali wakalamikia jambo fulani, basi ni vyema taasisi zinazohusika kulipitia. Kwa hivyo, wizara yangu imo katika mapitio ya suala hilo. Nina amini pengine wakati wa bajeti tutalizungumza kwa undani zaidi na tutatoa vigezo kama tumekubaliana na nyinyi au la. Nadhani tutafika kukubaliana kwa kiwango kizuri.

Tatu, Mhe. Spika, mita ni ghali mno, mita zinataka mamilioni ya fedha, tunao katika mpango. Hivi sasa tunaendelea kuwatilia wafanyabiashara kwa sababu ndio walipaji wakubwa. Baada ya hapo tutaanza kufika kidogo kidogo kuwatilia wananchi. Pia tunatizama teknolojia ipi itatufaa, kwa sababu kuna hatari pia ya watu kuchezea hizo mita zenyewe. Tutaingia katika gharama kubwa, halafu mita zenyewe zikawa rahisi sana kuchezewa tukapatata hasara juu ya hasara, wananchi wagumu wa kulipa, hapo hapo tukapatata hasara ya mita hizo tulizonunua. Kwa hivyo, linaendelea kufanyiwa utafiti na tutakuja kidogo kidogo.

Pia tulihisi tukiweka mita, kwa kweli mzigo kwa mwananchi utakuwa mkubwa sana, ndio maana tukasema tuweke *flate rate*, mita atalipa zaidi ya hizi Shs. 4,000/- na itakuwa ni ngumu sana kwa wananchi kumudu uwekaji wa mita. Kwa hivyo, ndio tukasema tuwape kwanza nafasi wananchi tuweke *flate rate*, tena hali ikitengamaa huko mbеле, hao watakaokuwepo watafanya maamuzi. Mhe. Spika, nakushukuru.

## Nam. 74

### **Maambukizi Mapya ya Virusi vya Ukimwi**

**Mhe. Ame Ussi Juma: (Kny: Mhe. Anacle Thobias Makungila) - Aliuliza:-**

Ni maeneo yepi mapya yanayotishiwa na maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi Zanzibar na kwa nini.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maeneo yote yanatishiwa na maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi hapa Zanzibar. Lakini maeneo ambayo ni hatari na kutisha zaidi ni kama ifuatavyo:-

- i) Maeneo yenyе kufanya biashara ya madawa ya kulevyя hasa watumiaji wa madawa hayo kwa njia ya kujidunga sindano.
- ii) Maeneo yenyе kufanya biashara ya ukahaba hususan watu wanaojiua miili yao.
- iii) Watu wanaofanya vitendo kinyume na maumbile.
- iv) Watu wanaobaka wenzao kwa makusudi ikiwa mmoja wapo ameambukizwa virusi kuna uwezekano mkubwa wa kuambukiza wenzao.

Mhe. Spika, ni vigumu kueleza eneo lipi ni hatari zaidi hapa Zanzibar. Jambo la muhimu ni kufuata maadili mema na kuepukana na mambo yote ya hatari yanayoweza kusababisha maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi nchini mwetu.

## Nam. 106

### **Viongozi wa Zanzibar Kutibiwa Nchini**

**Mhe. Ame Ussi Juma - Aliuliza:-**

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondosha.

## Nam. 46

### Upandaji Holela wa Bei ya Mafuta

#### Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Bei ya Mafuta duniani imepungua kwa kiwango kikubwa kutoka USD 146 kwa pipa hadi Novemba 2008, imefikia USD 62 kwa pipa. Hata hivyo, Wauzaji wa Mafuta hapa nchini wamepunguza Tsh. 100 tu kwa Lita moja ya mafuta hayo wanayowauzia wananchi wetu.

- (a) Kwa kuwa mafuta yakinapanda bei tu Ulimwenguni, wauzaji wa mafuta nchini hupandisha bei, lakini yanaposhushwa bei, wauzaji hawa wa nchi hii wanakuwa wagumu wa kushusha bei hiyo, Je. Mhe. Waziri Wizara ina mkakati gani wa kulitafutia ufumbuzi suala hili?
- (b) Kwa kuwa wizara inapaswa kukaa na wafanya biashara kwa lengo la kushauriana juu ya suala hili, Je. wizara imelichukulia hatua suala hili ?

#### Mhe. Waziri Nchi (ARBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 46 kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla, imekuwa ikilifua tilia kwa makini suala la kupanda na kushuka kwa bei za mafuta ulimwenguni. Ni kweli bei inapopanda wafanyabiashara wa bidhaa hiyo mara moja huleta malalamiko yao wizarani na serikali, ili bei ilipokuwa ikipanda wafanyabiashara husika kutaka bei ipandishwe. B=Ndipo Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), ambao ndio wasimamizi wa kodi zote za mafuta, pamoja na kupanga hizi bei za mafuta, hukaa pamoja na wafanyabiashara.

Hapa naomba kusisitiza Mhe. Spika, kwamba bei hizo sio kama (ZRB) wanapanga wao peke yao, lakini ni kwa mashirikiano. Tunakaa pamoja na makampuni ya kuingiza mafuta nchini, ili kujadiliana kwa pamoja na hatimaye kufikia bei muafaka, kuna vigezo vyetu ambavyo tunavifuata nitavitaja baadae. Halikadhalika, bei zinaposhuka ulimwenguni wizara inalizingatia

suala hili na pia hukaa nao hao waingizaji mafuta ili kutizama vipi tunaweza kushusha bei kutokana na hali halisi ya bei za mafuta zinavyoelekeza ulimwenguni.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba mnamo mwezi Julai, 2008, bei za mafuta zilipanda ulimwenguni hadi kufikia dola 147 kwa pipa moja la mafuta yasiyosafishwa (*Barrel* moja) hali hiyo ilipelekeza bidhaa za mafuta kupanda bei hadi kufikia lita moja ya mafuta ya *diesel* kufikia kuuzwa Tshs. 1,985 hapa nchini. Baada ya bei za bidhaa za mafuta kuanza kushuka ulimwenguni wizara ilichukua hatua mbali mbali, ili kuhakikisha kuwa bei za mafuta nazo zinashuka hapa nchini mwetu ambapo bei ya mafuta ya *diesel* hivi sasa imeshafikia kuuzwa kuuzwa Tshs. 1,410 kutoka Tshs. 1,985 kwa lita moja. Kwa hivyo, bei ya sasa imepungua kwa takriban Tshs. 575 kwa lita moja na sio Shs. 100 kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi.

Aidha, bidhaa nyengine za mafuta nazo pia bei zake zimeshuka kwa kiwango kinachofanana na mafuta ya *diesel*. Ni matarajio yetu kwamba bei hizo zitaendelea kushuka iwapo bei za bidhaa hizi zitaendelea kushuka ulimwenguni.

Hata hivyo, naomba izingatiwe kwamba hata kama bei za mafuta zitashuka kufikia dola 1 ya kimarekani kwa pipa la mafuta yasiyosafishwa, kuna gharama za bidhaa hizo kubakia pale pale, bei hizo ni kama ifuatavyo. Kwa sasa bei ya petroli ni Shs. 800, *diesel* Shs. 750 na mafuta ya Taa ni Shs. 352. Hizo ni gharama ambazo hata kama bei itashuka, basi hizi zinabakia, gharama zenyewe ni Kodi za Serikali, Usafirishaji, Bima, gharama za bandari, faida ya muagiziaji.

Suala jengine Mhe. Spika, lakuzingatiwa ni thamani ya pesa yetu ya Tanzania ukilinganisha na dola ya Kimarekani, ambapo wakati bei ya mafuta ya Julai 2008, dola 1 ya Kimarekani ilikuwa ni Shs. 1,180, wakati sasa imefikia kuwa Shs. 1,300. Hali halisi ilivyo wafanyabiashara wa mafuta wananaunu mafuta hayo ulimwenguni kwa dola, kadri shilingi yetu inapoanguka, basi wanapata hasara ya ununuzi wa mafuta hayo. Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kuwa hata kama bei ya mafuta itaendelea kushuka, basi kiwango chake cha kushuka hakiwezi kuenda sambamba na kushuka kwa kiwango hicho hapa nchini. Hali hii inachangiwa pia na kushuka kwa thamani ya sarafu yetu.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa bahati nilipoandika swali hili ulikuwa ni mwezi wa Novemba 2008, ilikuwa pipa moja la mafuta yasiyosafishwa yalikuwa yanauzwa dola 62, lakini leo linapojibowi swali hili Ijumaa ya tarehe 30/012009, pipa moja la mafuta linauzwa dola 36.

Je, pamoja na huo mtiririko mzima wa bei alioueleza Mhe. Waziri, lakini kuanzia mwaka huu mwanzo pipa moja lilikuwa dola 147 mpaka dola 36. Hivi kweli Mhe. Waziri haoni pamoja na mpango mzima wa usafirishaji na kila kitu, lakini bado Shs. 1,410 kwa *diesel* na Shs. 1,435 kwa petrol bado ni ghali.

Je, ana ushauri gani wa kuwashauri zaidi ili wapunguze bei wenzetu ili wananchi wanufaikie na gharama za daladala na usafiri mwengine.

**Mhe. Waziri Nchi (ARBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nina jadweli ndefu hapa, naomba univumilie kidogo nisome, ili nimpe mtiririko mzima Mhe. Ali Suleiman Ali, yeche naona alitoa ya mwezi mmoja tu, basi mimi ninayo ya miezi yote, kuanzia hapo aliposema yeche.

Aina ya Mafuta	Agosti, 2008	Septemba, 2008	Oktoba, 2008	Novemba, 2008	Disemba, 2008	Januari, 2009
MSP	1800	1800	1680	1680	1550	1435
GO	1985	1985	1840	1840	1680	1410

Mhe. Spika, sasa hii inaonesha *trend* kwamba kadiri hali ya mafuta yalivyokuwa yanapunguka na sisi tulikuwa tunapunguza. Lakini naomba kusisitiza tena yale masuala niliyozungumza kwamba hivi vigezo nilivyovisema kuwa, hasa katika suala la gharama za kuyaingiza nchini, wafanyabiashara wetu hawa wanalamakika. Mnajua wanapoleta mafuta kwa wingi kwenye makontena makubwa, basi gharama zake ni chache, lakini kwetu hapa mafuta yanayoletwa ni kwa kiwango kidogo, kwa hivyo gharama zake inakuwa ni kubwa, wanalamikia sana suala hili.

Vile vile kuhusu suala la kuanguka thamani ya sarafu ya pesa yetu. Nimetoa mfano, tulipoanza Shs. 1,180 na leo ni Shs. 1,300. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni lazima ujue kwamba inakubidi utoe pesa zako nydingi mfukoni ili kununua dola moja, hiyo ndio maana yake. Sasa hii inachangia sana Mhe.

Spika, bei kutoteremka ghafla, lakini bado ushauri wake tunauchukua na sisi kama nilivyosema tunaendelea kukaa na hao wafanyabiashara, hatupendi yale mambo ya kusukumana, zvia au panga bei. Matokeo yake tumeyaona Tanzania Bara juzi. Kwa hivyo, tunapenda tukae nao chini wenzenetu kama wafanyabiashara, wao wana *interest* ya biashara na sisi tuna *interest* na wananchi wetu.

Pia uliuliza swalii la kuhusu kuteremka bei kwa gharama za usafiri. Hilo nafikiri ni suala jengine, tumelisikia na nafikiri kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ambao nafikiri wanavyo vyombo hivi vyaa kutizama bei za vyombo vya usafiri vikoje. Basi sisi kama serikali tutakaa chini na kuona tunalifanya kazi. Ahsante.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ambayo aliyotoa Mhe. Waziri ya ufasaha, lakini naomba nimuuilize swalii la wakati. Mafuta yanapoteremka huwa yanachukua muda mrefu sana mpaka katika vituo kuteremka bei. Je, hii hasa huwa inasababishwa na kitu gani, kwamba serikali haijapata muda wa kukaa na makampuni, au inafaida kidogo katika kuzuia zvia inapata fungu lake kidogo, ahsante.

**Mhe. Waziri Nchi (ARBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Rashid Seif kwa kiwango fulani, kwamba mafuta yanapoteremka bei, basi ile kiwango cha kuteremka bei kwenye vituo haiwi kama kupandisha bei. Kupandisha bei pengine inapopandishwa tu basi pengine usiku ule ule, yanazuiwa yanapanda bei, lakini kushuka kuna matatizo yake. Nafikiri haya ni mambo ya kitendaji tu, na ile *enforcement* ya ile sheria, unajua tena binadamu ndio sisi. Lakini kwa kweli tangazo linatoka na wafanyabiashara wote wanajulishwa na wanatakiwa wachukuwe au wafute haraka utaratibu unaotakiwa. Lakini wengine watasingizia, aah! mafuta yetu tumalize, tungoje haya. Lakini inapoteremshwa ile bei tu, basi kuna wachunguzi wetu wanakwenda vituoni kule, wanapima mafuta yako kiwango gani. Kwa hivyo hata kodi itapunguzwa kwa mujibu wa mafuta yaliomo mule. Kwa hivyo, hiyo nasema ni mambo ya kitendaji tu.

## Nam. 47

### Ukwepaji wa Kodi Kwa Wamiliki wa Mahotel

#### Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Baadhi ya wawekezaji wa Mahotel nchini, hukwepa kulipa kodi kwa kubadilisha majina ya Mahotel yao, kila inapokaribia kumalizika muda wa msamaha wa kulipa kodi, jambo linaloikosesha mapato serikali yetu tukufu.

- (a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu ?
- (b) Kwa kuwa kuna wamiliki wengi wa Mahotel wanaotumia ujanja huu wa kukwepa kodi, Je, Wizara yako imechukua hatua zippi dhidi ya wakwepa kodi hawa ?
- (c) Je, kuna takwimu gani ya hasara iliyopatikana kwa serikali yetu, kutokana na kitendo hiki ?

#### Mhe. Waziri wa Nchi (ARBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 47 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeshajiisha sekta binafsi toka ndani na nje ya nchi kuwekeza katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kuongeza ajira kwa wananchi wetu na hivyo kuliongezea pato Taifa.

Mhe. Spika, chini ya sheria ya uwekezaji ya mwaka 2004, miradi inayowekezwa hupewa misamaha ya kodi, ikiwa pamoja na msamaha wa kodi ya mapato yatokanayo na faida ya kampuni yaani *Corporate Tax* kwa muda maalum kulingana na eneo la uwekezaji.

Aidha, Muwekezaji yoyote anayo haki kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji ya mwaka 2004 kuuza mradi wake wakati wowote anaopenda. Naye Muwekezaji aliyenunu mradi ana hiari ya kubaki na jina lile lile la mwanzo la mradi alonunu au kubadilisha jina na kuita jina jengine. Iwapo mradi ulipata msamaha wa kodi ya mapato ya muda maalum, haina maana kuwa kubadilika kwa mmiliki wa mradi, kunasababisha kutolewa kwa msamaha mwengine mpya kwa mmiliki mpya wa mradi.

Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa serikali kupitia Bodi ya Mapato Tanzania, (*TRA*) inakusanya kodi ya asilimia 10 ya faida, inayopatikana kutoka kwa mmiliki aliyeuza mradi wake wakati wa uuzaji wa mradi husika.

Aidha, kupitia *ZRB*, serikali hukusanya asilimia 1 ya bei ya ununuzi wa mradi kama ushuru wa stempu. *ZIPA* nayo hukusanya ada zake wakati wa kuidhinisha uhaulishaji wa mradi huo.

Mhe. Spika, sheria ya Makampuni, inaruhusu wamiliki wa Makampuni kubadili majina ya Makampuni na majina ya biashara. Hivyo Wawekezaji wanawenza kubadilisha jina la biashara la mradi na kutumia jina la biashara analoliona maarufu kwa ajili ya Mradi wake, lakini bila ya kubadilisha jina halisi la kampuni. Mara nyingi mabadiliko hayo hufanywa kwa kubadilisha jina la biashara yaani *Trade Name*, na kutumia jina la biashara lililo maarufu la kampuni kutoka nje ya Zanzibar, ili kuwavutia wateja wao.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine mabadiliko hayo yanaiongezea mapato serikali kwa kulipa kodi nyengine ya *Services Fees* ya asilimia 15 ya fedha zilizolipwa, kwa kutumia jina jengine maarufu la biashara la Kampuni maarufu ya nje ya nchi.

Kwa hivi sasa Mhe. Spika, serikali haina taarifa zozote za ukiukwaji wa kodi kunakosababishwa na Wawekezaji kubadilisha majina ya miradi, baada ya kumaliza muda wa msamaha wa Kodi ya Mapato. Hata hivyo, naomba nimuombe Mhe. Mwakilishi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote, kuisaidia serikali na wizara kama wanazo taarifa zozote za ukwepaji wa kodi wa aina hii, basi watujulishe na sisi tuko tayari kulifanya kazi.

## **HOJA YA KUONGEZWA MUDA WA MASWALI**

**Mhe. Spika:** Kabla ya kuendelea na maswali mengine ya nyongeza, tulikubaliana juzi kwamba kwa kuwa maswali yalikuwa ni mengi, basi tutenge kando taratibu za kanunua za kwenda na maswali mpaka kwenye saa 4:30 na kazi hiyo juzi ilianza hivyo. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe mnijulishe kama utengaji wa kanuni kando mlioufanya kama ulikuwa unajumuisha pamoja na leo. Lakini kama hivyo sivyo, na nafikiri mlifanya kwa siku ile tu peke yake. Lakini kama hivyo itakuwa ndivyo, yaani pamoja na leo tuendelee, na kama sivyo itabidi sasa tuombe Baraza liridhie kuongeza muda ili tumalize maswali yaliyokuwa mbele yetu, ili tufanye ile kazi ya kupunguza maswali ambayo Waheshimiwa Wajumbe mliyauliza, iwe kidogo tumeyapunguza. Nadhani tulifanya kwa siku ile tu peke yake. Ni sawa. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.

**Mhe. Waziri Nchi (ARBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, kwa kuwa kipindi cha maswali kinakaribia kumalizika, lakini maswali yetu bado hayajamalizika, basi naomba uweke kando kanuni hii na turuhusu tuendelee na maswali na majibu mpaka yatakapomalizika. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono. Wale wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Tunaendelea.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo wananchi wengi wamepata faida, hasa ya kuwa na shaka labda kuna utaratibu fulani wa ukwepaji wa kodi.

Mhe. Waziri kwa kuwa katika mahoteli kama haya yanayobadilishwa majina huwa yanawafanyakazi ambao alikuwa na jina lile la kwanza, lakini wafanyakazi wale wakiingia katika jina la pili, basi huwa wanaambiwa hapa utaratibu mzima wa uajiri wenu haupo na kwa kuwa wenzetu hawa wanakuwa na mfuko wa hifadhi ya jamii kule waliko.

Je, Mhe. Waziri hili atalichukulia hatua gani ili kuwaelimisha hao wanaonunua kwa sehemu ya pili ili wasiwaadhibu wafanyakazi hawa katika ajira zao.

**Mhe. Waziri Nchi (ARBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nakubaliana naye Mhe. Ali Suleiman kwamba haya yanatokezea. Lakini ninachoomba, nafikiri Mhe. Asha Abdallah mara nydingi anazungumza suala hili la mikataba kwa wafanyakazi wetu kwa waajiri. Tujitahidi sana tuwaelimishe na tuwatake wananchi wetu wanapoajiriwa basi wajitahidi sana kujaza mikataba, hilo ndio suala la msingi sana.

Pia makampuni nayo kama alivyoshauri, tutajitahidi na kuwaelimisha na kuona kwamba vipengele kama hivi vinafanyiwa kazi. Kwa sababu tumegundua kwamba haya mambo yanatokezea mara kwa mara ya kuuza miradi yao. Kwa hivyo, tutawataka wawaingize kwenye mikataba wafanyakazi wao, pindi ikitokezea mambo kama haya viyi waweze

kuwasaidia wafanyakazi hawa juu ya masuala yao ya hifadhi ya jamii, ahsante.

### Nam. 93

#### **Ushiriki wa Wananchi Katika Uanzishaji Jumuia ya Afrika Mashariki**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: (Kny: Mhe. Salmin Awadh Salmin)**  
– Aliuliza:-

Tokea kuanzishwa kwa Jumuia ya Afrika Mashariki kumekuwa na vikao mbali mbali vya wanachama vinavyofanyika kuanzia ngazi za watendaji hadi ngazi za wanasiasa. Kwa kuwa vikao hivi ndivyo vinavyopanga mambo mbali mbali ya Kijumuia. Kwa kuwa watendaji wetu wa Zanzibar mara nyingi huwa hawashiriki katika vikao hivyo ipasavyo. Kwa kuwa sababu zinazoleenza za kutoshiriki kwao ni ukosefu wa fedha ama kuchelewa kupata taarifa kutoka kwa wenzetu wa Tanzania Bara.

- (a) Je, Mhe. Waziri, hivi serikali inaelewa kuwa kutokushiriki katika vikao hivyo kuanzia ngazi za watendaji kunaikosesha Zanzibar fursa ya kueleza misimamo yetu juu ya jambo lilinalojadiliwa ?
- (b) Je, serikali inachukua hatua zipi katika suala zima la ukosefu wa fedha za ushiriki wa vikao muhimu vya Jumuiya ?
- (c) Je, serikali imefanya juhudu gani katika kuhakikisha kuwa taarifa za vikao zinafika mapema iwezekanavyo, sio kama ilivyo hivi sasa

**Mhe. Waziri wa Nchi (ARMBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 93 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali nikiri inaelewa kwamba kutoshiriki katika vikao vya Jumuia ya Mashariki kuanzia ngazi ya watendaji, kunaweza kuikosesha Zanzibar fursa ya kueleza misimamo yetu juu ya jambo linalojadiliwa katika vikao hivyo ?
- (b) Kutokana na kuelewa umuhimu huo wa kushiriki katika vikao hivyo, basi serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua kila hatua, ili kuhakikisha kwamba watendaji wetu wanashiriki

kikamilifu katika vikao hivyo. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na mambo yafuatayo ?

- 1) Kuwashimiza watendaji wetu kufuutilia tarehe za vikao vinavyowahusu, ili kuzielewa mapema na kuweza kupeleka maombi yao ya mahitaji ya fedha kwa wakati na kwa hivyo kuipa nafasi Wizara ya Fedha na Uchumi kuwaingizia fedha zinazohitajika kwa safari za watendaji hao.
- 2) Wizara ya Fedha na Uchumi inaelewa umuhimu wa Zanzibar kushiriki katika vikao hivyo vyta Jumuia. Kwa hivyo, wizara hiyo inatoa kipaumbele kadiri inavyowezekana kwa maombi ya fedha kwa ajili ya kuhudhuria vikao hivyo.
- 3) Serikali imeshachukua hatua kwa kushirikiana na wizara ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuhakikisha kwamba katika vikao vya kamati vya wataalamu ambazo zinalipiwa na Secretarieti ya Jumuia, wataalamu wa Zanzibar na wao wanakuwemo na kulipiwa gharama za safari zao.

Nafikiri juzi tulimsikia Mhe. Waziri anayeshughulika na Jumuia ya Afrika ya Mashariki, dokta Kamala, ambaye alikiri kabisa kwamba kuna wataalamu waliopo kwenye Secretarieti ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki wanalipwa na wao Jumuia moja kwa moja. Kwa hivyo, niseme kwamba wataalamu wa Zanzibar na wao wanakuwemo na tayari wameshakuwemo.

- (c) Tatizo la kuchelewa kupata taarifa za kuhudhuria mikutano ya Jumuia ni tatizo linalozikumba serikali za nchi zote wanachama. Katika vikao vya hivi karibuni vya Jumuia suala hili lijadili na likatolewa maamuzi kwamba serikali itoe mialiko ya mikutano mapema iwezekanavyo, ili kuzipa serikali hizi wakati wa kutosha wa maandalilzi.

Kwa kiasi fulani tatizo hili linaonekana kupungua kutokana na maamuzi ya pamoja na nchi zote wanachama. Hata hivyo, juhudhi zinaendelea kuchukuliwa ili kuondoshwa kabisa tatizo hili, ahsante.

## Nam. 67

### **Mashamba ya Umwagiliaji kwa Wawakilishi**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) – Aliuliza:**

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira katika kushiriki wito wa kitaifa wa upatikanaji wa chakula na kuondoa njaa nchini ina mpango gani wa kuwapatia mashamba ya umwagiliaji maji Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao washiriki kikamilifu kuitikia wito huo ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swalı lake Nam. 67 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba maeneo ya wakulima ya umwagiliaji maji yote yako chini ya dhamana ya kamati maalum za mabonde husika. Hivyo, baadhi ya maeneo ya umwagiliaji maji unafanywa na jumuia kuu ya bonde husika.

Ninawashauri Wajumbe wa Baraza hili tukufu ni vyema kufika na kuonana na kamati za mabonde, ili kupeleka maoni yao kwa ajili ya kupatiwa maeneo.

Isipokuwa wizara yangu ina jukumu la kutayarisha mabonde hayo kitaalamu na kukabidhi kamati hizo kwa ajili ya ugawaji.

## Nam. 72

### **Sheria Inayokataza Uvuvi wa Samaki Wadogo**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) – Aliuliza:**

Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini imepiga marufuku kwa mtu yeoyote kuvua na kuchukua kushusha, kuuza, kupokea au kumiliki samaki yoyote mwenye ukubwa chini ya ule uliowekwa kwa aina yoyote ya samaki na endapo amevuliwa kwa bahati mbaya ni lazima arejeshwe majini mara moja na kuwa uwezekano mdogo wa kuumia au kuathirika.

(a) Je, ni sheria ipi na ya mwaka gani iliyopiga marufuku mambo hayo

- (b) Samaki wenye ukubwa chini ya ule uliowekwa bado wanaendelea kuvuliwa na kuonekana sokoni, madikoni, mitaani na kadhalika. Idara ya Uvubi na Mazao ya Baharini inachukua hatua gani kuzuia au kuokoa samaki wadogo wasiendelee kuangamia ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 72 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Sheria ya Uvubi Nam. 8 ya mwaka 1988 kifungu cha 6 (1) (d) inapiga marufuku kuvuliwa na kuwa bado au kuuza samaki wenye ukubwa chini ya ule uliowekwa kisheria.
- (b) Ni kweli kuwa samaki wenye ukubwa chini ya ule uliowekwa kisheria bado wanaendelea kuvuliwa na kuonekana. Idara ya Uvubi na Mazao ya Baharini inachukua hatua za kuzuia na kuokoa samaki wadogo wasiendelee kuangamia kwa kuzingatia taratibu zifutazo:-
- (i) Kuendelea na utoaji wa taaluma kwa wavuvi ikiwa pamoja na kuwafahamisha umuhimu wa kutovua samaki wachanga.
- (ii) Kuendelea na doria kwa mashirikiano na vyombo vyta ulinzi KMKM na Jeshi la Polisi katika kufanya doria za baharini.
- (iii) Mipango ya kuanzisha doria za aridhini na madikoni iko mbioni, ambapo kwa kiasi kikubwa itawenza kufanikisha jitihada za kupambana na wavuvi waharibifu.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Hatua zinazochukuliwa na wizara ya Kilimo ni pamoja na kutoa elimu kwa wavuvi. Lakini maeneo yetu ya bahari hasa magharibi ya kisiwa chetu ambayo yanapakana na Tanzania Bara, huvuliwa na wavuvi wa pande zote wa Bara na Visiwani. Kwa upande wa Zanzibar elimu inatolewa. Je, hawa wenzetu wa bara tunaovua pamoja wizara inahakikisha vipi na wao wanapata taaluma kama hii wanayoipata wavuvi wa Zanzibar ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, kwa wavuvi wenzetu wale wanaotoka Tanzania Bara pamoja na kwamba hatuwapati kwa ajili ya kuwapa taaluma. Lakini pale tunapowakamata wakati wanapofanya uvuvi haramu, suala kubwa tunalolichukulia hatua ni kuwafikisha kwenye vyombo nya kisheria bila ya kujali wanatoka upande gani.

Lakini suala la kupata taaluma au laa wavuvi wa upande wa Tanzania Bara, hili tutalifuatilia na tutamjibu kwa maandishi.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu naomba kuuliza swalii moja la nyongeza. Katika jibu lake mama Mhe. Naibu Waziri amesema suala la kuvua samaki wadogo ni marufuku, lakini wako samaki maumbile yao ni madogo wakiwemo dagaa, medo mkondo na wengineo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri angeweka wazi kwamba samaki asivuliwe chini ya nchi mbili. Lakini akisema samaki wadogo anaweza kuwagombanisha wasimamizi wa uvuvi na wavuvi.

Kutokana na hali hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri atueleze kigezo cha samaki mdogo ni kipi na wale wanaofaa kuvuliwa ni kipi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, kwa kweli kuna samaki ambaye amemtaja kwa jina la kishamba na hapa Barazani tunatafautiana lahaja na wala sikumfahamu. Lakini kuhusu samaki wadogo kama vile dagaa wa aina ya saladini, hawa hatujapiga marufuku na wanaendelea kuvuliwa.

Tunaowakusudia ni wale wanaokuwa wakubwa wakiwemo changu, pono na wengineo wale ndio tuliofiga marufuku. Kwa hivyo, hatuna nia ya kuwagombanisha wavuvi. Sambamba na hilo wakuu wa madiko nao pia wameelekezwa na wanajui ni samaki wa aina gani waliopigwa marufuku na serikali.

Vile vile ni matumaini yetu ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tuliwahi kupata semina na tulielekezwa umuhimu wa kupata samaki mdogo na baadaye kupata samaki mkubwa. Kwa hiyo, tulipata fursa ya kuona samaki tangu kiluilui, samaki wa kawaida na baadaye anakuba samaki mkubwa kwa ajili ya kuvuliwa na kuweza kunufaika.

## Nam. 31

### Kukatazwa Mashindano ya Urembo

#### Mhe. Ali Denge Makame (Kny: Ramadhan Nyonje Pandu) – Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni serikali ilikataza na kupiga marufuku Mashindano ya Urembo ya (Ma-Miss), lakini siku chache zilizopita kulifanyika Mashindano ya Maonesho ya Mavazi hapa Zanzibar katika Hoteli ya *Africa House* yaliyoandaliwa na *EXPLORE ZANZIBAR* na kuwashirikisha warembo wengi.

- (a) Nini tofauti kati ya Mashindano ya Mavazi na Mashindano ya Urembo ya (Ma Miss) yaliyokataliwa na kupigwa marufuku.
- (b) Ni kwa dhana gani iliyoshukiwa na seikali ya kukataza Mashindano ya Urembo na kwa dhana gani iliyokubaliwa na serikali kuendesha Mashindano ya Mavazi wakati wote wanaonesha urembo wa sura zao na wanaonesha uzuri wa mavazi yao watakuwa na mantiki ileile ya kuwa warembo na kuweza kuvutia na kushawishi nafsi za watu wengine wawapende ama kwa sura au mavazi yao.

#### Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la Nam. 31 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli serikali ilipiga marufuku Mashindano ya Urembo hapa Zanzibar. Vile vile napenda kumhakikishia kuwa msimamo wa serikali kuhusu mashindano hayo bado upo pale pale na wala haujabadilika.

Pili naomba nikubaliana naye kuwa ni kweli hivi karibuni palifanyika Maonesho ya Mavazi katika Hoteli ya *Africa House* na kuwashirikisha akina dada wengi.

- (a) Mhe. Spika, tofauti ya msingi uliopo baina ya Maonesho ya Urembo na Maonesho ya Mavazi, ni kuwa haya Maonesho ya Urembo yanalenga kwenye uzuri wa sura na umbo la msanii, na haya Maonesho ya pili ya Mavazi yanalenga kwenye uzuri wa vazi na ushoni wa nguo aliovaa msanii huyo.

Kutokana na tofauti hiyo vigezo vya kuingilia kwenye mashindano hayo navyo pia vinatafautiana. Msanii anayetaka kushiriki kwenye Maonesho ya Urembo kutokana na wataalamu wa fani hiyo hupimwa kwa vigezo vya uzuri wa umbile la mwili, sura, miguu, nywele, ngozi, kucha, misuli na kadhalika na misuli kwa wanaume kwa wale wanaoshiriki urembo.

Lakini kwa yule anayetaka kuingia kwenye Mashindano ya Mavazi yeeye hupimwa kwa kigezo cha kupendezwa na nguo aliovaa jinsi vile nguo ilivyoshonwa, usanii uliotumika katika usanii huo. Hata hivyo, sura yake na umbile pamoja na viungo vyengine huwa si muhimu sana katika mashindano haya.

Matokeo ya mashindano haya yanatafautiana sana. Katika Mashindano ya Urembo msanii mwenyewe huwa ndiye mshiriki ambaye anayetakiwa kushindwa, lakini kwenye Mashindano ya Mavazi mshindi huwa lile vazi lenyewe lililosonwa kwa mtindo fulani na wala sio mtu, bila ya kujali iwapo aliyeavaa vazi hilo ni mwanamke au mwanamme ama sura yake inavutia au umbo lake linavutia, isipokuwa huwa ni vazi lenyewe.

- (b) Mhe. Spika, serikali imepiga marufuku Maonesho ya Urembo kutokana na ukweli kwamba unamdhaliisha mwanadamu na hasa mwanamke. Kwa hivyo, tathmini ya uteuzi hufanywa kwa wasanii kupitia kwenye jukwaa liloinuka wakiwa nusu maungo wazi, ili umbo pamoja na maumbile yake mengine yawefe kuonekana kwa uzuri huo unaoangaliwa kwa wakati huo.

Kwani tathmini ya uteuzi pia hufanywa kwa wasanii kupitia jukwaa hilo liloinuka na hii Mhe. Spika ni kinyume na silka, mila na hata utamaduni za Mzanzibari kwa watoto wetu wa Kizanzibari na hususani watoto wa kike.

Mhe. Spika, maadili ya Wazanzibari yanaona wanawake wote kuwa wanao uzuri unaolingana na hivyo hivyo kwa wanaume. Kutokana na mtazamo huo na mantiki hiyo ndipo serikali ikaona hakuna haja ya kuruhusu Mashindano ya Urembo kufanyika hapa Zanzibar na badala yake ni Mashindano ya Mavazi tu ndiyo yanayoruhusiwa kufanyika.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Je, Mhe. Waziri haoni kuwa uzuri wa vazi ni vile lilivyomjaa mvaaji ?
- (b) Kama yanayoshindanishwa ni mavazi kwa nini hayatundikwi yale mavazi na watu wakayaangalia na kuona lipi zuri au baya ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika,

- (a) Kwanza kabisa ni kweli vazi au linatathminiwa na hao wataalamu wa fani hii kutokana na yule aliyeavaa hilo ninakubaliana. Kwa mfano, tunaweza kusema Mhe. Zahra Ali Hamad hatizamwi urefu wala ufupi wake, isipokuwa kinachoangaliwa pale ni ile vazi alilovaa na siku zote anapendeza na vazi lile linampendeza. Kwa hivyo, hapo ni vazi moja kwa moja.
- (b) Amesema kwa nini vazi lile lisitundikwe tu na kuangaliwa pale dukani na tayari ule urembo ndio umeshakamilika. Mhe. Spika, wataalamu wa fani hii kama ilivyo kwa wachoraji na wasanii wengine, huwa wanasema lazima ikae mwilini. Kwa mfano, Mhe. Moh'd Ali Salim ameveaa kofia, kazu leo siku ya Ijumaa pamoja na koti, lakini pengine vitu hivyo angeavaa mwengine ingekuwa tofauti. Kwa hivyo, vazi lazima lilake mwilini, ili lioneokane na sio kwenye henga wala kutundikwa (*Kicheko*).

### Nam. 32

#### Haja ya Mabadiliko katika Vyombo vyta Habari

**Mhe. Ali Denge Makame (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu) – Aliuliza:-**

Kutokana na kuwepo kwa vyombo vingi vyta habari binafsi hapa nchini, waandishi wa Habari wa Vyombo vyta Serikali wanakabiliwa na changamoto kubwa ya utendaji wa kazi, ili kuvifanya Vyombo vyta Habari vyta Serikali vihimili ushindani wa hali ya juu kutoka Vyombo vyta Habari Binafsi.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba serikali inahitaji kufanya mabadiliko makubwa katika masuala yafuatayo:-

- (i) Ajira,
- (ii) Utoaji habari,
- (iii) Teknolojia ya mawasiliano,
- (iv) Vitendea kazi na

- (v) Uwezeshaji (kuwawezesha) waandishi wake kiutendaji.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa ni kweli serikali inahitaji kufanya mabadiliko makubwa katika vyombo vyake vyaka habari kuhusiana na masuala yafuatayo:-

- (vi) Ajira,
- (vii) Utoaji habari,
- (viii) Teknolojia ya mawasiliano,
- (ix) Vitendea kazi na
- (x) Uwezeshaji (kuwawezesha) waandishi wake kiutendaji.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeyaona hayo yote na imeanza kuchukua hatua zifuatazo:-

- (a) Kuhusu suala la ajira hivi sasa wizara yangu tayari imeshaziagiza idara pamoja na taasisi zake zote kuzingatia suala la uajiri kwa upande wa ajira, yaani waajiriwe vijana wasomi na wenye vyeti, shahada pamoja na kutokana na sheria ziliwekwa za habari.
- (b) Utoaji wa habari ni eneo jengine ambalo limepewa kipaumbele hasa kwa kuanzia kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2008/09. Wizara yetu ya habari kupitia Tume ya Utangazaji tayari imeshafanya mikutano miwili tofauti na wamiliki wa Vituo vya Utangazaji Binafsi na vile Serikali katika afisi yao iliopo Migombani, ili kujadiliana na kuandaa taratibu za kushughulikia suala la utoaji wa habari na utangazaji wa vipindi bora kwa kuamsha ari ya kupambana na umasikini na kuleta maendeleo hapa Zanzibar.
- (c) Mhe. Spika, matumizi ya teknolojia ya mawasiliano yamechukua hatua mpya hasa katika vyombo vyaka habari kwa uingizaji na matumizi ya komputa, *internet* pamoja na vifaa vyengine vyaka teknolojia vyaka *digital* katika kukusanya, kupokea, kuchapisha na kusambaza habari hizo.

Gazeti la Zanzibar Leo hivi sasa linatayarisha utoaji wa toleo lake la kila siku kwa kutumia teknolojia hii mpya kama walivyokuwa wameanza wenzetu kwenye maendeleo.

Vile vile matayarisho kama hayo ya kutayarisha habari na kuzipeleka hewani kupitia vyombo veya utangazaji pia zinafanyika kwa kutumia teknolojia hii mpya. Kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya teknolojia hii ya habari na mawasiliano kwa makusudi kabisa Wizara ya Habari imeingiza vipengele vinavyoolekeza malengo pamoja na mikakati ya matumizi yake katika mwaka huu.

- (d) Mhe. Spika, ningependa kujibu kipengele cha nne na tano katika swali Nam. 32 kwa pamoja, kwa sababu maswali mawili haya yanawiyana na kwenda pamoja.

Wizara inaendelea na juhudi zake za kuwapatia mafunzo mbali mbali watendaji wake ndani na nje ya nchi. Pia inaendelea na utaratibu wake wa kuzipatia taasisi zake za bahari vifaa bora na vitendea kazi ikiwa pamoja na vipaza sauti, vyombo veya usafiri kwa ajili ya kutafutia habari na kuyafanyia ukarabati majengo yanayotumiwa na waandishi hao, ili waweze kufanyakazi katika mazingira safi na salama.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu tuliyopewa ambayo yanaridhisha kiasi, nataka kujua pamoja na kwamba wametakiwa waboreshe katika hali hizi zilizoelezwa hapa.

Je, Mhe. Waziri haoni pia kama ipo haja vyombo vyetu kuptitia wizara hii kuitangaza Zanzibar zaidi kuliko kutegemea vyombo veya nje. Kwa mfano, kwa mara ya kwanza juzi tulikuwa na Mahafali ya kuwatunuku Vyeti veya Diploma katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, tulitegemea tuone vyombo vyetu vimechukua sehemu kubwa kama sio yote. Je, hili pia liwe ni wajibu mkubwa kwao.

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa majibu ya swali la nyongeza kuhusu Mahafali ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilichopo Maruhubi. Kwa hivyo, ye ye angependelea vyombo vyetu vingechukua sehemu kubwa mahafali yale kwa sababu ni ya Zanzibar na vyombo vyetu vingeonesha mambo mengi ya Zanzibar kuliko kuonesha mambo mengine.

Mhe. Spika, nakubaliana na wazo hilo, lakini inaonekana kwamba Mhe. Mjumbe hakuangalia kipindi chetu cha televisheni. Kama alikusudia kuoneshwa *alive* kama wanavyosema watu hivi sasa, hilo halikufanyika. Isipokuwa kulikuwa na kipindi kilichooneshwa kwa muda mrefu na mimi mwenyewe shahidi nilikiona na tulionesha Mahafali yale ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Vile vile chombo chetu kimeonesha mahafali ya Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu, pia na mahafali ya Chuo Kikuu Kishiriki Chukwani. Kwa hivyo, tunaelewa kwamba ni wajibu yale mazuri yanayotendeka hapa Zanzibar hasa kwa vijana wetu pamoja na mafanikio yao yaoneshwe, ili wananchi wape faraja ya kutosha. Kwa maana hiyo, hilo linafanywa.

Isipokuwa kama kuna mapungufu ambayo angedhani yangeongezewa na kujaliziwa, ili hilo likatendeka ubora zaidi, basi tuko tayari kusikiliza ushauri wake. lakini hususan mahafali ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar yalioneshwa kwa ukamilifu.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Ninaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuititia wizara hii, kwa sisi wawakilishi wa vijijini kule katika kila siku setu kwa Mkuu wa Wilaya tumepatiwa mwandishi wa habari mwenye ujuzi pamoja na cheti.

Lakini waandishi wa habari hawa wanashindwa kufanya kazi ipasavyo, kutokana na hali ya usafiri pamoja na mazingira ya maposho maalum kwa ajili ya kuwasaidia kama kitendea kazi. Kutokana na hali hiyo, habari zinazotoka hivi sasa ni za Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wabunge pamoja na Wawakilishi kwa sababu wanambeba yule mwandishi wa habari kwenye gari zao, lakini taasisi nyengine pamoja na watu wengine ambapo kunakuwa na habari mbali mbali ambazo ni nzuri katika jamii nafasi hiyo hawana.

Je, Mhe. Waziri atatusaidia vipi kuhusu suala hili kuona waandishi wa habari wanawezeshwa kutoa taarifa za wananchi wengine, kwa sababu hii ni haki ya kila mtu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba kweli tunalo tatizo la usafiri kwa hawa maafisa wa waandishi waliokuwepo mpaka ngazi ya wilaya. Suala hili tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala wa Mikoa na Vikosi vya SMZ, kwa sababu wale wanakuwa upande mmoja wa Tawala za Mikoa na Wizara ya Habari ambayo wanawajibika moja kwa

moja. Kwa hivyo, tutalifanya kazi na pale uwezo utakapoturuhusu tutajitahidi japo baskeli wapate.

## Nam. 61

### **Juhudi za Waandishi wa Habari Kuelimisha Jamii kuhusu UKIMWI na Madawa ya Kulevyaa**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Kny: Anaclet Thobias Makungila)**  
– Aliuliza:-

Waandishi wa Habari wa hapa Zanzibar wanachukua juhudi gani za kuelimisha jamii juu ya ongezeko la ugonjwa wa UKIMWI na ongezeko la matumizi ya madawa ya kulevyaa na madhara yake badala ya kujikita zaidi na masuala ya siasa na michezo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Kitengo cha Habari Kamisheni ya UKIMWI (ZAC) ndicho chenyeye jukumu la moja kwa moja katika suala la kuelimisha masuala ya UKIMWI hapa Zanzibar.

Hata hivyo vyombo vyoma habari Zanzibar ni moja ya sekta iliyo mstari wa mbele katika kuelimisha wananchi kuhusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutumia njia mbali mbali kwa mashirikiano ya karibu mno na Tume ya UKIMWI Zanzibar.

Mhe. Spika, mbali ya kuweka matangazo ya kawaida ya kila siku kwenye Sauti ya Tanzania Zanzibar, Televisheni ya Zanzibar pamoja na Gazeti la Zanzibar Leo, pia vyombo hivyo huwa na vipindi maalum kuhusiana na mapambano hayo kwa kushirikiana na wataalamu kutoka taasisi mbali mbali za serikali ikiwemo Tume ya UKIMWI Zanzibar.

Kwa mfano, hivi sasa ni zaidi ya mwezi mmoja huwekwa makala moja ya taaluma katika Gazeti la Zanzibar Leo kila wiki kuhusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI hapa Zanzibar.

Aidha michezo ya kuigiza, ngonjera pamoja na sanaa nyengine za maonesho kusikika moja kwa moja katika radio zetu za Sauti ya Tanzania Zanzibar na kuonekana katika Televisheni ya Zanzibar pamoja na Gazeti la

Zanzibar Leo. Kwa madhumuni ya kuelezea mapambano dhidi ya madawa ya kulevyo, ambayo nayo hupewa nafasi kubwa kwa Waandishi wa Vyombo vyta Habari vya Serikali kutokana na kuelewa kuwa hilo ni jukumu lao kwa jamii wanayoifanyi kazi moja kwa moja.

### Nam. 43

#### **Hoteli ya Kiweni Resort**

**Mhe. Hasnuu Moh'd Haji** – Aliuliza:-

- (a) Hoteli ya Kiweni Resort iliyojengwa huko Mwambe na Mwekezaji wa Afrika ya Kusini na baadaye kuondoka bila ya kukamilika na kuanza kazi sasa amepewa mwekezaji gani.
- (b) Serikali inafaidikaje na hoteli hiyo iliyopo bila ya kufanya kazi hadi sasa.
- (c) Kwa nini boti mbili za hoteli hiyo zinaachwa na kuendelea kuharibika bila ya kushughulikiwa tafauti na boti zinazokamatwa na magendo ambazo hunadiwa kwa wananchi.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, kwanza napenda kukiri kwamba kweli mradi huo upo na hivi sasa haufanyi kazi. Hata hivyo, naomba nieleze historia fupi ya mradi huo.

Mradi ulijengwa kwa ubia baina wa wawekezaji wageni kutoka Norway na Denmark kwa kushirikiana na mwekezaji wa Kitanzania. Kwa bahati mbaya mmoja wa wawekezaji wa kigeni alifariki dunia, hali ambayo iliufanya mradi huo kukosa ufanisi na baadae kafilisika kabisa. Hali hii ililazimisha Benki waliyokopa fedha za awali kwa ruhusa ya Mahkama kuuza hoteli hiyo na kurejesha fedha zao.

Hoteli hiyo pamoja na vitu vyote vikiwemo hizo Boti zilizoulizwapamoja na vifaa vya ujenzi vilinunuliwa na Mwekezaji wa Kitanzania ambaye anamiliki hoteli ya *Super Lodge* ambapo hivi sasa ni mmiliki halali wa hoteli hiyo. Ujenzi wa hoteli hiyo umesita kutokana na eneo la mwanzo la mradi huo kuonekana kwamba ni dogo na ameomba kuongezewe eneo.

Hii ni sababu kubwa ya kusita ujenzi wa hoteli hiyo kwa vile bado ombi lake liko katika taasisi husika.

- (b) Mwekezaji huyo analipa kodi ya ardhi (*land lease*) ya mradi huo kila mwaka wakati akisubiri ombi lake la kuongezewa eneo la mradi kukubalika au kukataliwa.
- (c) Boti ambazo zipo ni sehemu ya mradi huo. Kwa hivyo, wenye mradi ndio wanaozitumia boti hizo.

**Mhe. Hasnuu Moh'd Haji:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri anatambua kwamba hoteli ilipojengwa kuna wafanyakazi wasiopungua 50 hadi leo hawajapewa haki zao?

Kama anatambua je, wizara itawasaidia nini vijana hao?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, nilikuwa natambua kwamba kulikuwa kuna mgogoro wa madai katika eneo o lile au katika mradi ule wakati nikiwa Waziri wa Kazi. Kwa wakati ule suala hili tulishughulikia ipasavyo na kwa sasa hivi najua kuna wafanyakazi wasiopungua wanne ambao wamewekwa kulinda eneo hilo. Kwa hivyo, sina hakika kama mpaka leo kuna wafanyakazi ambao hawajapata haki zao. Kwa sababu najua wakati nilipokuwa Waziri wa Kazi tulishughulikia madai yao.

**Mhe. Mohammed Ali Salim:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, naomba njue ni muda gani sasa tangu huyo mwekezaji mpya aliyenunua alipoomba kuongezewa eneo?

Pili, kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji unahitajika muda gani mpaka aweze kupata majibu?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kipindi cha miaka isiyopungua minne toka wawekezaji wa mwanzo wamekorofishana na kuuzwa hoteli hiyo. Katika kipindi cha mwaka mzima wa mwanzo toka mwekezaji mpya amenunua alikuwa anafanya *survey* ya eneo lile pamoja na kuijandaa ni mradi wa aina gani anaweza kuujenga. Lakini ni kipindi cha miaka miwili sasa toka ameombwa kuongezewa eneo na hili sitaweza kulitolea majibu mazuri kwa sababu uongezaji wa eneo ni jukumu la Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na sio wizara yangu.

Kwa upande wa wizara yangu kuititia *ZIPA*, huwa tunamtaka mwekezaji atueleze maendeleo anayofikia kila baada ya miezi sita, mara ya mwisho tumekutana naye tayari ametayarisha michoro ya mradi ambao anataka kuujenga. Kwa hivyo, tunajua kwamba yuko kwenye *process* lakin bado hajafanikiwa kuongezewa eneo. Hajafanikiwa kuongezewa eneo kwa sababu, katika eneo alilolichukua kuna mradi mwengine upo kati kati, kwa hivyo alikuwa ana ni-*negotiate* na muwekezaji mwengine ambaye na yeze ana eneo na ameanza kujenga aweze kumnunua aondoke ili huyu apate eneo kubwa zaidi. Lakini vyenginevyo hata kama ataongezewa eneo inabidi apewe eneo ambalo amenunua amruke muwekezaji mwengine halafu aongezewa eneo upande wa pili na haya sio matakwa yake.

Kwa hivyo bado wanaendelea *ku-negotiate* na muwekezaji huyu ambaye yuko kati kati ahsante sana.

**Mhe. Kamal Basha Pandu:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

- a) Mhe. Waziri amesema katika maradi huu kuna muwekezaji mzalendo, naomba kuuliza kwamba. Je, katika uuzwaji wa hoteli hii muwekezaji mzalendo amefaidika au ameathirika kwa kiasi gani.
- b) Hisa hii imeingia kwa muwekezaji wa pili au imeruka.

**Mhe. Waziri Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, muwekezaji mzalengo ambae alikuwa ni mke wa mmoja katika wawekezaji wawili wale na baada ya mumewe kufariki mgawanyo ulifanywa sawa sawa na mwenye shea huyu alipata sehemu yake kama alivyostahiki, kwa hivyo na yeze alifaidika.

## Nam. 76

### Utalii na Utamaduni

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila – Aliuliza:-**

Hivi ni kweli kwamba ujio wa watalii huharibu utamaduni wa nchi husika kwa vijana kuiga utamaduni wa nchi za nje kama vile mavazi, nyimbo na madawa ya kulevyo nk.

## **Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza yatupasa tuelewe kwamba si kila Nchi yene Utalii, Utamaduni wake kuharibiwa na utalii, lakini unaweza kuwa ni chachu muhimu ya kuendeleza utamaduni wa nchi husika. Inatupasa kuelewa kuwa utamaduni ni bidhaa (*product*) muhimu sana katika kuendeleza utalii na ndio maana nchi ikiwemo Zanzibar huhifadhi utamaduni wake ili kuvutia watalii zaidi.

Mhe. Spika, si kweli kwamba uingizaji wa watalii unaharibu utamaduni wa Nchi husika lakini ni umakini wa jamii na vyombo vyta ndani ya nchi vinavyopaswa kusimamia utamaduni ndivyo vinavyosababisha utamaduni wa nchi husika kuharibika.

Mhe. Spika, tuna mifano ya nchi zilizoendelea sana kiutalii kama Tunisia na Egypt lakini utamaduni wao haujaharibika, lakini pia kuna vivutio au vichangizi vyengine vyta mitandao, televisheni na mambo mengine ndio yanayosababisha vijana wetu kukopia au kuiga mambo ambayo hayamo ndani ya utamaduni.

Jengine kubwa kama tulivyolizingumza juzi wakati tunazungumza sheria ya bodi ya sensa ni uingiaji wa wageni nchini hawakai muda mfupi lakini wanakaa kwa muda mrefu ndani ya nchi, hawa nao huja na tamaduni zao na kuchangia kubadilisha utamaduni wa nchi husika.

Mhe. Spika, Sheria ya bodi ya sensa tulivoipitisha juzi na kamati zake zilizomo ndani zitatusaidia kwa kiasi kikubwa kurudisha hadhi ya utamaduni wa Zanzibar. Kwa hivyo ningechukua nafasi hii kuwaomba waheshimiwa wawakilishi nasi tukakaza kamba katika maeneo yetu tulikotoka, kuwafanya vijana kutokuiga utamaduni wa nje zaidi bali tudumishe utamaduni wetu kwani ni kivutio kikubwa kwa utalii wetu hapa nchini.

Kubwa zaidi ningechukua nafasi hii kuwaomba wazazi nao kuhakikisha kwamba vijana hawatupotei, kupitia hatua hizo tunaweza kudumisha utamaduni wetu na ukawa ni kivutio kikubwa kwa utalii wetu wa Zanzibar.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini hata

hivyo naomba anisaidie kujibu wali langu la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo.

- a) Kwanza Mhe. Waziri katetea kwamba watalii sio wanaoleta madhari lakini kuna taasisi nyengine ndio zinazochangia suala hili. Sasa napenda kujua nani mwenye jukumu la kuwazuia wale watalii wanaotembea utupu ambaao sasa hivi wameenea hapa Unguja.
- b) Kuna hawa ndugu zetu wengine kutoka nje ya Zanzibari ambaao vile vile siku hizi nao wanatembea utupu hapa, kwa kiasi fulani wale watalii wanaokuja kutoka nje hawajui kama hawa ni Wazanzibari au sio Wazanzibari na inawezekana wakaondoka na mawazo kwamba haya mavazi wanayovaa ndio mavazi ya Kizanzibari.
- c) Je, nani hasa anayehusika kwa kuwazuia hawa Watanzania wanaotembea utupu ambaao watalii wanaweza kuwafikiria ni Wazanzibari.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, Mwenye jukumu la kuwadhibiti wanaokwenda kinyume na sheria za nchi kwanza wasimamizi wa sheria za nchi ni Jeshi la Polisi, lakini pia sisi wananchi wenye nchi hii au wana jamii ni busara tukatumia sheria tulizokuwa nazo na kulinda utamaduni wetu. Lakini tatu ni serikali na serikali ni kuanzia ngazi ya sheha, katika shehia zetu hawa watu tunawakodisha majumba, tunaishi nao na tunawaona kwa hivyo kama sisi ni jamii tungeweza kuwadhibiti kuanzia ngazi ile aidha kuwarekebisha waendane na yale ambayo tunayataka sisi, au kama hawawezi kuwarekebisha basi kuripoti katika vyombo vinavyohusika.

Lakini kuna Idara nzima ya utamaduni ya hapa Zanzibar nayo kwa kiasi fulani ina jukumu la kudhibiti utamaduni wetu.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kati ya utalii na utandawazi kwa maana ya *Inter net* kipi kinachoharibu utamaduni zaidi?.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, utalii ni sekta ambayo inaingiza mambo mengi, inawezekana kuna mtu anakuja kutalii kwa kusoma utamaduni wa Zanzibar tu uko vipi, kuna mtu anaweza

kuja kwenye mkutano akaondoka ni mtalii, kuna watalii wanaokuja kuangalia mambo mbali mbali.

Lakini mara nygingi tunavyozungumza utalii tunakwenda kwenye utalii wa anasa zaidi kuliko sehemu nyengine, kwa hivyo ni kweli kwamba kuna utalii wa anasa lakini unafanyika sehemu maalum ambako kumepangwa mambo yale kufanyika.

Lakini tukizungumzia utandawazi au mambo ya *internet* na mambo kama hayo kuna vijisehemu sehemu vingi ambavyo vijana wetu wanaweza kwenda wakafungua na kuona, sasa hapa somo hili au mada hii inaendana na matakwa ya mtu mwenyewe unaweza kuangalia *internet* kutoka asubuhi mpaka usiku lakini akili isikutume kuiga kama una maadili ya nchini kwako au kama una silka, maadili na malezi mazuri ya Zanzibar. Kwa sababu kuna mambo ya mchanganyiko wa watu unaweza kuona yale na kuiga, sasa suala lako ni kwamba kati ya utalii na utandawazi upi unaharibu zaidi.

Mimi nataka kusema utandawazi unaharibu zaidi kwa sababu unaona, unasoma na unaweza kuiga pale pale, kwenye utandawazi unapata maelezo mengi zaidi ya kuiga kitu, lakini kwenye utalii kama ni kumuangalia mzungu unamuangalia tu kakupitia kavaa nguo nusu ukitaka kumuiga kesho ni akili yako mbovu, lakini ukiona kavaa kapita ni hiari yako. Lakini utandawazi unapata mpaka maelezo ya nini kifanyike, nini ufanye, uanze hatua gani ufanye vipi kwa hivyo utandawazi unaharibu zaidi kuliko utalii.

## Nam. 80

### **Ushughulikiaji Wa Bidhaa Zilizopitwa na Muda**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:**

Kwa kuwa taasisi ya Mwenendo wa Biashara na kumlinda mtumiaji ndio yenye jukumu la kuhakikisha kwamba maduka na maghala hayana bidhaa zilizopitwa na muda kwa matumizi ya binaadamu.

- (a) Mhe. Waziri kwa kuwa taasisi hii ni muhimu sana katika kulinda afya za wananchi, ni lini Serikali inafikiria kuwapatia vitendea kazi vyta kisasa ikiwa ni pamoa na vipando na vipimo.
- (b) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba uhaba wa wataalam, na ukosefu wa Mkemia Pemba kunaathiri shughuli za taasisi hii katika kisiwa cha Pemba.

## Nam. 43

### Hoteli ya Kiweni Resort

**Mhe. Hasnuu Moh'd Hajji**

-

Aliuliza:-

- (a) Hoteli ya Kiweni Resort iliyojengwa huko Mwambe na Mwekezaji wa Afrika ya Kusini na baadaye kuondoka bila ya kukamilika na kuanza kazi sasa amepewa Mwekezaji gani.
- (b) Serikali inafaidikaje na hoteli hiyo iliyopo bila ya kufanya kazi hadi sasa.
- (c) Kwa nini boti mbili za Hoteli hiyo zinaachwa na kuendelea kuharibika bila ya kushughulikiwa tafauti na boti zinazokamatwa na magendo ambazo hunadiwa kwa wananchi.

### **Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

- a) Kwanza naomba ieleweke kwamba baada ya kupitisha bodi ya madawa, vyakula na vipodozi kazi ya kuangalia hadhi ya ya chakula sasa inafanywa na taasisi mbili, lakini kwa kiasi kikubwa inafanywa na bodi ya madawa, vyakula na vipodozi ikishirikiana na idara ya kumlinda mtumiaji, hata hivyo ndani ya mradi wa kulinda mtumiaji kuna mradi ambao tumeuwasilisha katika shirika la maendeleo la mataifa la UNDP chini ya mradi wa JPC mradi huu unahusu kuimarisha kitengo cha kumlinda mtumiaji ndani ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na ndani yake kuna mafunzo na ununuvi wa vifaa pamoja na vyombo nya usafiri.
- c) Ni kweli uhaba wa wataalam na ukosefu wa Mkemia Pemba huasiri shughuli za taasisi hii katika kisiwa cha Pemba, hasa ukizingatia kwamba kuna vyakula vyengine havipiti bandari ya Zanzibar ndio vikapelekwa Bandari ya Pemba lakini vinapita katika bandari ndogo ndogo za Pemba, kwa hivyo kwa muda huu chakula kinakaguliwa hapa Unguja halafu ndio kinakwenda Pemba, lakini kwa kileambacho kinapita bandari ndogo ndogo za Pemba huwa hakikaguliwi na Mkemia Mkuu.

Kwa hivyo hilo nakubali kwamba ni tatizo na niseme tu kwamba kitengo cha kumlipa mtumiaji tutajitahidi kushirikiana na Wizara ya Afya ambayo ndio yenye bodi ya vyakula madawa na vipozozi pamoja na jukumu la mkemia mkuu, kwa hivyo tutajitahidi kushirikiana nao ili tulitafutie ufumbuzi tatizo hili kwa kule Pemba.

#### **Nam. 4**

##### **Ukataji wa Bima Kwa Vituo vya Mafuta**

**Mhe. Ali Denge Makame (Kny: Mhe. Ali Abdalla Ali)** – Aliuliza:-

Shirika la Bima limeanzishwa kwa lengo la kumsaidia mwananchi kupata usalama wa mali na maisha yao kwa kuzingatia aina ya bima aliyojiwekeea mwananchi huyo, ikiwa ni pamoja na Bima ya ajali, moto, na biashara.

- (a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba vituo vingi vya biashara ya mafuta (Sheli za mafuta) havina Bima.
- (b) Kwa kuzingatia hatari ya ajali ya moto inayoweza kutokezea ambayo itasababisha athari kwa wamiliki wa vituo hivi na jamii kwa ujumla, Je Wizara yako ina mpango gani wa kuzuia athari hizo.
- (c) Kwa kuwa ukataji wa Bima upo kisheria, je hakuna kifungu chochote cha Sheria kinachowataka wamiliki wa vituo vya mafuta kukata Bima ili kuepusha athari ambazo zingeweza kutokea.
- (d) Kama kifungu hicho kipo, ni hatua zipi zilizochukuliwa na Wizara kuhakikisha kwamba, wamiliki hawa wanafuata sheria hiyo.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Wizara inafahamu kwamba ni muhimu vituo vya mafuta kukata bima, lakini kutokana na takwimu tulizopata kutoka Shirika la Bima la Zanzibar ni vituo sita tu vya mafuta ndio vilivyokata bima pale na hivi ni vituo vya watu binafsi, lakini kuna uwezekano mkubwa kwamba vituo vya mashirika kama

GAPCO, ZP na UP vimekata bima kwa majina ya kampuni zao kupitia taasisi nyengine za Bima.

Mhe. Spika, kama nilivyofafanua mwanzo narudia tena kusema kwamba Wizara yangu inaelewa umuhimu wa vituo vy a mafuta kukata bima lakini bahati mbaya sheria ya bima haina kifungu kinachomlazimisha mfanya biashara kukata bima ile, wanachokifanya ni kuelimisha wafanya biashara na kuwaelekeza manufaa na madhara ya kutokuwa na bima au manufaa ya kukata bima. Kwa kipengele hicho wizara yangu pia haina nguvu za kisheria ya kukaa na wafanya biashara na kuwalazimisha wakate bima.

## KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi Rais Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya leo zimemalizika na kwa kuwa Waziri Kiongozi anahitaji wakati kidogo ili kukamilisha hotuba yake, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liahirishwe kabla ya wakati wake.

**Mhe. Spika:** Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubali hoja hiyo wanyanyue mikono mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa. 5.15 Baraza lilahirishwa mpaka Saa. 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

## TAARIFA MAALUM

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe Kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri Kiongozi ili kutoa hoja ya kuahirisha Mkutano wetu naomba kwanza nitoe taarifa na pengine kabla ya taarifa hiyo nichukue nafasi hii kwa mara nyengine tena kuwashukuru wajumbe wote kwamba tulikuwepo katika Mkutano wetu huu wa 14 ambao tunategemea kuufunga leo hii kwa mashirikiano makubwa, utulivu mkubwa, nidhamu kiasi cha kwamba imewezesha shughuli zetu kwenda vizuri. Kwa hivyo, nakushukuruni Waheshimiwa Mawaziri,

Waheshimiwa wenyeviti wa kamati mbali mbali, Waheshimiwa Wajumbe kwa ujumla, watendaji wetu wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi bila ya kuwasahau watendaji wa serikali ambao walikuwa wanakuja kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri wao kwa shughuli ambazo ziko mezani.

Lakini pia shughuli zetu zimekuwa zimefahamika vyema na kutangazwa kwa wananchi kuititia vyombo vyetu vya Redio na Televisheni ya Zanzibar, kwa ujumla kazi hiyo imekwenda vizuri kutokana na waandishi wa habari ambao walikuwa nasi kwa muda wote. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa kiasi cha kuwezesha shughuli zetu zikaweza kwenda vizuri.

Pili nichukue nafasi hii kutoa taarifa fupi ambayo itakamilisha shughuli muhimu ambayo tunategemea kwa siku ya tarehe 1 siku ya Jumapili. Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwatangazia na kuwaarifu rasmin kwamba hitma na arubaini ya Marehemu Mhe. Daudi Hassan Daudi aliyejewa mwakilishi wa jimbo la Magogoni itafanyika siku ya Jumapili tarehe 1/2/2009 baada ya sala ya Adhuhuri katika Msikiti wa Mwembeshauri kwa upande wa wanaume. Kwa upande wa wanawake hitma hiyo na arubaini itafanyika siku hiyo hiyo ya Jumapili ya tarehe 1/2/2009 baada ya sala ya Adhuhuri Kijangwani nyumbani kwa baba wa marehemu karibu na Kituo cha Polisi cha Ng'ambu. Nafikiri mtakumbuka pale ambapo maiti alitoka nyumbani kwa marehemu karibu na kituo cha Polisi Ng'ambu hapo ndio Waheshimiwa wanawake wanaalikwa waende hapo.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe naomba kuchukua nafasi hii kukuombeni nyote kwa pamoa muhudhurie katika shughuli hiyo ili kuonyesha mapenzi yetu kwa mwenzetu ambaye ameshatangulia mbele ya haki na tuweze kumuombea dua kwa Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi, Amin.

Baada ya hapo Mhe. Waziri Kiongozi karibu.

## **KUAHIRISHWA BARAZA**

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenyerehema kwa kutuwezesha kutekeleza kwa ufanisi

mkubwa shughuli za Baraza lako tukufu. Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuuendesha mkuutano huu kwa umahiri na umakini wa hali ya juu. Tatu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za serikali na kutoa maoni mbali mbali wakati wa kujadili hoja zilizowasilishwa hapa Barazani. Mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri maswali yalioulizwa pamoja na kutoa ufanuzi wa hoja mbali mbali.

Katika mkuutano huu jumla ya maswali 79 yaliulizwa na kujibowi na Waheshimiwa Mawaziri. Vile vile, Baraza lilijadili na kuipitisha miswada mitatu ya Sheria. Halikadhalika, Wajumbe wa Baraza walipata fursa ya kushiriki katika semina mbili.

Mhe. Spika, Miswada iliyowasilishwa Barazani ni kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu na Maonesho.
2. Mswada wa Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.
3. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar.

Mhe. Spika, mswada wa kwanza kujadiliwa na Baraza lako tukufu ulikuwa wa sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho. Mswada huu unapendekeza utaratibu wa kudhibiti utengenezaji na uingizaji wa filamu na michezo ya kuigiza ili kulinda na kuhifadhi mila, utamaduni na desturi za Zanzibar. Hatua hii itaisaidia sana kuhakikisha kuwa filamu na michezo ya kuigiza na kazi za sanaa kwa ujumla hazipotoshi maadili ya watu wa Zanzibar.

Hapana shaka mswada wa sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa ya filamu na maonyesho umekuja katika wakati muwafaka sana ambapo tunashuhudia kuongezeka kwa utengenezaji na uingizaji wa filamu zisizofaa kutoka nje ya Zanzibar. Pamoja na kwamba utengenezaji wa filamu na michezo ya kuingiza ina umuhimu mkubwa katika kukuza sanaa lakini suala hili linaweza kuleta athari kubwa kwa jamii yetu hasa iwapo filamu hizi hazina ubora unaotakiwa. Ni ukweli ulio dhahiri kuwa kwa muda mrefu hatukuwa na utaratibu mzuri wa kuangalia ubora wa filamu kabla hazijaonyeshwa hadharani. Kutokana na kutokuwepo kwa utaratibu huo wa kuhakiki filamu na michezo mengine ya sanaa imekuwa ni vigumu sana kujua filamu hizo zinawafaa watu wa rika gani.

Hivi sasa ni jambo la kawaida sana, kuona filamu za watu wazima zinaangaliwa na watoto au vijana walio chini ya umri wa miaka 18. Hili ni jambo linalosikitisha sana kwa sababu linaharibu malezi ya watoto wetu. Wakati mambo yote hayo yakiendelea kufanywa kama yanavyofanywa tunatupia lawama watoto kuwa hawana maadili mema. Nakumbuka zamani Televisheni Zanzibar kwa mfano ilikuwa na utaratibu maalum wa kupanga filamu na vipindi kwa kuzingatia umri wa watazamaji yaani kulikuwa filamu maalum na vipindi vya watoto na watu wazima. Leo hali haiko hivyo. Watoto wanaangalia filamu na vipindi vyote pamoja na watu wazima. Watoto hawa wanatumia muda wao mwangi kuangalia Televisheni. Hali hii inasababishwa na mambo mawili makubwa.

Kwanza, wazazi wenyewe hawawadhibiti watoto wao kuangalia vipindi vya Televisheni. Mtakubaliana nami kwamba wanasaikolojia wanatueleza kwamba jambo hili si tu linaathiri maadili ya jamii bali pia linaathiri maendeleo ya kielimu ya watoto hao. Uzoefu unaonyesha kwamba watoto wanaotumia muda mwangi kuangalia Televisheni baadhi yao hawafanyi vizuri katika masomo yao kwa sababu wanakosa muda wa kutosha kudurusu masomo.

Pili, inawezekana watayarishaji wa vipindi wameuacha utaratibu wa kupanga vipindi kwa kuzingatia rika ama kutokana na ujuzi mdogo au kutokuwa na muda wa kutosha katika kupangilia vipindi kitaalamu.

Sisi wazazi na walezi tunao wajibu mkubwa sana kurekebisha tabia za watoto wetu. Katika siku za hivi karibuni baadhi ya walezi wanawatumia watoto kwa mfano kwenda kukodi filamu na michezo mengine isiyo faa. Tabia hii haina tofauti sana na ile ya mtu mzima kumpa mtoto sigara akawashe na halafu akuletee. Bila shaka mtoto anayetumwa sigara awasge na amletee mtu mzima hupata vishawishi vya kuvuta sigara yeze mwenyewe. Hivyo hivyo mtoto anayepewa uhuru wa kukodi filamu ama na watu wazima wengine au na mlezi, siku moja atakodi filamu yeze mwenyewe zisizostahiki na kuanza kuziangalia. Halafu sisi walezi watoto watakapojifunza mambo mabaya tutaanza kuwalauku.

Mhe. Spika, siku hizi imezuka tabia ambayo si nzuri sana ya utengenezaji wa filamu kuwaonyesha wanawake kama chombo cha kuwastarehesha watu hadharani. Vitendo hivi vinawadhalilisha sana akina mama. Nyinyi ni mashahidi na mimi ni shahidi kwamba katika baadhi ya filamu hasa zile zenye ngoma wanawake wanaonyeshwa wamevaa nguo zisizoridhisha hata kidogo wakati wanaume wao huвая nguo za heshima hili jambo linashangaza sana. Wakati mwengine wachezaji wa kike wa ngoma wanatikisa miili yao kiasi cha

mtu anayejiheshimu kushindwa kuwaangalia na kama kuna mtu karibu basi mtakuwa hamuangaliani usoni. Vile vile wasanii wanaonyesha vitendo nya ngono ama kwa sauti au ishara katika filamu zao. Watazamaji wa filamu hizi wakubwa na wadogo hawapati shida kupata taswira ya wanachokiona au kusikia katika filamu hizo. Kutokana na kukithiri kwa mambo haya Bodi ya sensa ya filamu na maonyesho ina wajibu mkubwa wa kudhibiti mambo haya ili tuweze kulinda mila, desturi na silka za Zanzibar.

Mhe. Spika, mswada wa pili uliojadiliwa ulikuwa ni ule wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Mswada huu unakusudia kukibadilisha Chuo cha Ufundii cha Karume kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Hatua hii inakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya kuimarisha mafunzo ya Sayansi na Teknolojia hapa Zanzibar. Ni dhahiri kuwa mafunzo yatakayotolewa katika taasisi hii yatakuwa na mchango mkubwa sana katika kukuza vipawa nya ugunduzi na ubunifu mionganini mwa vijana wetu. Sayansi na teknolojia itawajengea uwezo vijana wa kutengeneza vifaa mbali mbali na kufanya utafiti wa kina wa kisayansi. Shughuli hizi zitasaidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta maendeleo kwa jumla kama ilivyo katika nchi za India na Malaysia nchi ambazo zenye mazingira ambayo hayatofautiani sana na ya kwetu.

Mhe. Spika, sayansi na teknolojia ina umuhimu mkubwa katika kukabiliana na mazingira yaliyomzunguka binaadamu. Ninatoa mfano mmoja kuonyesha jinsi sayansi inavyosaidia kubadilisha mazingira yanayotuzunguka. Mtakumbuka katika miaka ya nyuma maeneo ya Pete na Jozani yalikuwa na ndorobo wengi sana waliyokuwa wakiathiri mifugo ya wananchhi wa maeneo hayo. Hali hii iliathiri ufugaji katika eneo hilo. Mnamo miaka ya tisini utafiti wa kitaalamu ulifanyika na kugundua kuwa ng'ombe wa sehemu hizo walikuwa wakisumbuliwa na maradhi ya malale ambayo yanasaababishwa na ndorobo. Kwa hivyo, watalam wa Zanzibar wakishirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki walibuni mbinu za kisayansi za kutumia mionzi kuwahasi ndorobo dume ili kuzuia uzazi na hatimaye kuwaangamiza ndorobo hao.

Dk. Hans Blix aliyekuwa kiongozi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la nguvu za Atomiki wakati huo ambao walikuwa ndio wafadhili wakuu wa mradi huu alisema. "Mafanikio haya yameiweka Zanzibar katika ramani ya dunia kama nchi iliyofanikiwa kuangamiza ndorobo kwa mbinu za kisayansi." Mafanikio haya yalisababisha wanasyansiyi mashuhuri duniani kuja hapa Zanzibar na kutembelea Jozani kushuhudia jinsi Zanzibar ilivyo fanikiwa kutumia sayansi kukabiliana na matatizo ya ndorobo. Kutokana na mafanikio hayo hivi sasa

wananchi wa jozani maeneo hayo wanafuga ng'ombe wao bila ya matatizo yoyote. Mafanikio haya ni mfano wa kielelezo cha umuhimu wa sayansi katika kutatua matatizo yanayowakabili wanaadam katika jamii.

Mhe. Spika, kama Zanzibar inataka kupiga hatua za maendeleo siku zijazo haina budi kutilia mkazo mafunzo ya sayansi na teknolojia. Kwa kutambua umuhimu wa Sayansi na Teknolojia katika kuleta maendeleo, Serikali ya Mapinduzi imeamua kuimarisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Taasisi hii itakuwa na malengo yafuatayo:-

- (i) Kusambaza elimu ya Sayansi na Teknolojia kwa kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri.
- (ii) Kuandaa mafunzo ya Sayansi na Teknolojia katika ngazi mbali mbali ili kukidhi mahitaji ya Zanzibar katika soko la ajira ndani na nje ya nchi yetu.
- (iii) Kutoa vyeti, stashahada na shahada za masomo ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe waliosema kuwa nia njema ya serikali ya kuanzisha taasisi ya sayansi na teknolojia peke yake haitoshi. Lazima serikali iwe na dhamira ya dhati kuongeza kiwango cha bajetiya Wizara ya Elimu ili kuiwezesha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na vyuo vingine kutekeleza majukumu yake vizuri. Sote tunaelewa kuwa taasisi hii inahitaji walimu wenye ujuzi, maabara na karakana zenye vifaa vya kisasa ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji. Ili tuweze kufikia malengo yote haya serikali haina budi kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu kila mwaka. Tutajitahidi sana kuongeza bajeti ya elimu kila mwaka kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. Hili ni jambo muhimu sana kwa mustakbali wa taifa letu hapo baadaye.

Mhe. Spika, mswada wa tatu kujadiliwa ulikuwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar. Mswada huu unakusudia kutunga sheria inayounda Mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa sheria namba 5 ya usafiri wa baharini ya mwaka 2006. Zanzibar ina nafasi kubwa sana ya kukuza sekta ya usafiri baharini hasa tukizingatia kuwa Zanzibar ina historia ndefu katika sekta hiyo. Kwa miaka mingi Zanzibar imekuwa ikitumia vyombo vya baharini kusafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu mbali mbali za dunia. Kwa mantiki hiyo serikali ina wajibu mkubwa

wa kusimamia usalama wa vyombo na kuhifadhi mazingira ya bahari. Ili kusimamia suala hilo mamlaka ya usafiri wa baharini imepewa uwezo wa kuzuwa vyombo visivyofaa kusafirisha abiria na mali zao na kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaohatarisha usalama wa vyombo hivyo au kutupa takataka za sumu baharini. Utaratibu huu ukisimamiwa vizuri utatusaidia sana kuimarisha usalama wa wananchi wanaotumia vyombo nya baharini.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali pamoja na kujadili miswada ya sheria Waheshimiwa Wajumbe pia walipata fursa ya kuhudhuria semina mbili na kujadili masuala ya uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki na Sekta ya Bima Tanzania. Katika semina ya uanzishaji wa Soko la Pamoja Wajumbe walielezwa hatua zilizofikiwa katika maandalizi ya uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Tulielezwa kuwa hivi sasa wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wanaendelea kuondoa vikwazo nya biashara ili kila nchi mwanachama inufaika na ushuru wa Forodha. Utaratibu huu unatarajiwu kuweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa soko la pamoja hapo baadaye.

Hivi sasa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaendelea kujadiliana kuhusu namna ya kuanzisha soko la pamoja. Wakati wanachama wengine wakitaka uwepo uhuru mpana wa kumiliki ardhi, kutoa ajira na uhaniaji kutoka nchi moja kwenda nyengine, Tanzania inayapinga sana mawazo haya. Tanzania inaamini kuwa hakuna mahali popote duniani palipokuwa na uhuru wa kufanya biashara, kuhamisha mitaji na kuhamia sehemu nyengine ya nchi bila ya mipaka. Kwa mantiki hiyo, jambo hili linahitaji kuwekewa utaratibu unaostahiki.

Mhe. Spika, kabla nchi wanachama hawajaanzisha rasmi Soko la pamoja, zinapaswa kuwa makini katika umiliki wa ardhi kwa sababu huu ndio urithi tulioachiwa na wazee wetu na kuangalia pia na kuweka utaratibu wa kuwa na pasi za kusafiria badala ya kuacha tu utaratibu holela. Nawaomba wananchi hasa wa Zanzibar waendelee kutoa maoni yao bila ya hofu kila fursa ya kufanya hivyo inapopatikana kujadili masuala ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, narejea wito nilioutoa katika semina ya wiki iliyopita, Watanzania na hasa Wazanzibari tunapaswa kuwa makini sana katika kuilinda ardhi yetu na kuwasomesha vijana wetu ili waweze kushindana katika soko la ndani na nje.

Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka wakati wa kujadili masuala haya mlitoa mawazo mazuri sana na ya kina. Wajumbe kwa ujumla wao walitoa ushauri katika maeneo matatu yafuatayo:-

1. Waliishauri, Serikali ya Mapinduzi kuhakikisha kuwa Zanzibar haiwekewi vikwazo vya aina yoyote ya biashara na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili iweze kufaidika na fursa za kibiashara.
2. Zanzibar inyanyue kiwango cha elimu ili vijana wake waweze kumudu ushindani katika soko la ajira.
3. Zanzibar ipewe upendeleo maalum ili kuwa bandari huru ili kukuza biashara. Zanzibar ipewe upendeleo maalum wa kuwa na bandari huru kama ilivyo Dubai kwa nchi za Falme za Kiarabu.

Mhe. Spika, serikali itafanya kila linalowezekana kuyafanyia kazi mawazo haya ili Zanzibar iweze kunufaika na fursa zilizomo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki vyengingevyo tutakuwa kama wasindikizaji tu.

Mhe. Spika, semina ya pili tuliyopata fursa ya kuhudhuria ilikuwa inahuu Sekta ya Bima Tanzania. Sekta ya Bima inaendelea kukua kwa kasi na kuchangia katika kukuza pato la taifa. Pamoja na kukua kwa sekta hii hapa Zanzibar, imebainika kuwa sehemu kubwa ya mchango wa bima inategemea sana bima ya magari. Wataalamu wa masuala ya bima walitueleza kuwa kasoro hii inainyima Zanzibar mapato ya uhakika. Kwa sababu bima ya magari ina mapato madogo kuliko bima ya maisha. Vile vile Shirika la Bima Zanzibar halijaweza mpaka sasa kuwashawishi wawekezaji wakubwa wa hoteli za kitalii kukata bima zao hapa Zanzibar na badala yake wawekezaji hao wa hoteli wanakata bima zao Shirika la Bima Tanzania au wanafanya hivyo kwa mashirika ya bima nje ya Tanzania. Jambo hili linapaswa kuangaliwa kwa makini kwa sababu linatupotenza mapato makubwa sana.

Mhe. Spika, kadri siku zinavyokwenda ndivyo biashara ya bima inavyoendelea kukabiliwa na ushindani wa hali ya juu. Ili kukabiliana na ushindani huu vyuo vikuu vya Zanzibar vinapaswa kuanzisha masomo kuhusu masuala ya bima. Hatua hii itawaongezea wafanyakazi ujuzi na maarifa katika masuala ya bima. Serikali

itajitahidi kushirikiana na Shirika la Bima Zanzibar ili liweze kufikia malengo iliyojipangia. Naliomba Shirika la Bima la lizingatie ujuzi na utaalamu wakati wa kuwaajiri wafanyakazi wao ili kuongeza tija na ufanisi kazi.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu miswada na semina sasa nachukua fursa hii kutoa maelezo ya utekelezaji wa shughuli za Taasisi za Serikali. Katika mkutano wa 13 wa Baraza hili nilieleza hatua zinazochukuliwa na serikali katika kufanikisha zoezi la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki hapa Zanzibar. Kutowana na umuhimu wa suala hili nimeamua kulieleza tena Baraza lako tukufu juu ya mafanikio na matatizo tunayokabiliana nayo katika zoezi hili.

Bila shaka tumepata mafanikio ya kuridhisha katika kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Kwa mujibu wa taarifa za kiukaguzi kutoka Idara ya Mazingira, hivi sasa kuna mifuko ya plastiki michache katika maghala ya biashara ya mifuko hiyo. Wananchi wengi wameanza kutumia mifuko ya karatasi, vitambaa na kurejesha utamaduni wetu wa kutumia mikoba ya ukili. Hatua hii inaelekea italeta faraja kwa wajasirimamali wadogo wadogo. Wajasirimamali hawa wameongeza kipato chao kwa sababu soko la mikoba na mifuko ya karatasi limeongezeka sana. Naliomba Wizara ya Biashara ikutane na wafanyabiashara ili kutafuta uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mifuko isiyoharibu mazingira hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na kupiga marufuku uuzaaji na matumizi ya mifuko ya plastiki bado baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kuuza mifuko hiyo kwa siri sana kwa ajili ya kufungia samaki, mikate, au matunda. Serikali inaendelea kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaopinga amri hii. Mpaka sasa jumla wafanyabiashara 95 wamefunguliwa kesi na kati ya hao 84 wameshahukumiwa na wamepeewa adhabu ya faini kati ya Tsh.50,000/- na 70,000/- na kesi tisa bado ziko Mahakamani.

Mhe. Spika, ingawa kwa kiasi fulani mifuko ya plastiki imepungua sana lakini bado kuna baadhi ya wananchi wanazitumia bandari zisizo rasmi kuitisha bidhaa hizo kutoka Tanzania Bara na Kenya. Inawezekana kabisa baadhi ya wafanyabiashara wanaihifadhi mifuko

ya plastiki katika nyumba zao. Kwa hivyo, natoa wito kwa watu hao kuacha kabisa kuuza mifuko ya plastiki na waliokuwa nayo hivi sasa nawaomba waisalimishe Baraza la Manispaa au Idara ya Mazingira. Nawashukuru wananchi wanaotekeleza amri hii ya serikali kwa kukataa kuuziwa mifuko hiyo. Nawaomba sana wananchi waendelee kutotumia mifuko hiyo ili kuepuka usumbufu usio wa lazima. Naviomba vyombo vinavyohusika hasa polisi wawakamate wauzaji na watumiaji wa mifuko hiyo kwa kukaidi amri hii.

Mhe. Spika, jambo jengine nililolizungumza katika mkutano uliopita ni suala la maendeleo ya soko la Saateni. Kwanza, natoa shukurani zangu za dhati kwa wafanyabiashara na wananchi walioitikia wito wa serikali wa kuhamia katika soko la Saateni hasa wafanyabiashara wa mitumba. Kama mnavyokumbuka wafanyabiashara waliokuwa wakifanya biashara katika eneo la Darajani linalojulikana kwa jina la Jua Kali walisababisha usumbufu mkubwa kwa watu wanaopita katika eneo hilo. Ili kuweka utulivu katika eneo hilo serikali iliamua kuwahamishia wafanyabiashara hao katika soko jipya la Saateni. Kwa batî mbaya baadhi ya wafanyabiashara walipinga uamuzi huu kwa sababu walidai hawatafanya biashara nzuri katika soko jipya. Naendelea kuwanasihi wafanyabiashara hao wakubali kufanya biashara zao huko Saateni na si vyenginevyo.

Mhe. Spika, ninayo furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa wafanyabiashara wanaendelea kufanya biashara zao vizuri sana katika soko jipya la Saateni. Kutokana na kushamiri kwa biashara katika soko la Saateni Baraza la Manispaa linakusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara na taarifa nilizonazo mpaka sasa Baraza hilo linakusanya kati ya shilingi 1,800,000/= na shilingi milioni mbili kwa mwezi. Makusanyo hayo bado ni madogo sana lakini Baraza hilo limeniahidi kuwa litaongeza makusanyo zaidi situ zijazo. Kutokana na makusanyo ya mapato katika masoko mbali mbali Baraza la Manispaa limeweza kulipa deni lake kwa mfuko wa hifadhi ya jamii. Mpaka sasa Baraza la Manispaa limebakisha deni la shilingi 14 milioni kati ya shilingi 300 milioni zilizokopwa kutoka mfuko wa hifadhi ya jamii. Deni hili linatarajiwa kulipwa mwishoni mwa mwezi ujao. Nachukua nafasi hii kulipongeza Baraza hilo kwa kazi nzuri walioifanya.

Mhe. Spika, bado tunaendelea kutekeleza miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Kama mnavyolewa utekelezaji wa awamu ya pili ulianza mwaka 2006 na unatarajiwa kumalizika mwaka huu wa 2009. Mpaka sasa utekelezaji wa miradi hii unakwenda vizuri.

Siri kubwa ya kufanikiwa kwa utekelezaji wa miradi hii ni kubuniwa kwa mpango wa kuwashirikisha wananchi katika kupanga na kuteua miradi wanayoipenda kutokana na mahitaji yao na kuacha utaratibu wa zamani wa wafadhili kuwachagulia wananchi miradi. Kabla ya kubuni mpango wa kuwashirikisha wananchi katika kupanga miradi na kuteua miradi, miradi mingi iliyokuwa ikifadhilna na wafadhili ilikuwa kwa sababu wananchi walihisi kuwa miradi ilioanzishwa ilikuwa sio yao ilikuwa ni miradi ya washirika wa maendeleo. Ndio maana baada ya wafadhili wa miradi kuondoka miradi hiyo mingi ilikuwa katika baadhi ya maeneo.

Ili Mfuko wa Maendeleo ya Jamii uweze kutekeleza miradi ya maendeleo umepatiwa dola za Kimarekani 2.56 milioni kutoka Benki ya Dunia. Vile vile mfuko huu umepatiwa dola za Kimarekani 1.5 milioni kutoka Tume ya UKIMWI kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo. Halikadhalika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umepatiwa dola 3.2 milioni kutoka *MACEMP*. Jumla ya fedha zilizotolewa kwa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ni dola milioni 7.26.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu tokea kuanza utekelezaji wa Miradi ya *TASAFII* hapa Zanzibar wananchi wamepata mwamko mkubwa wa kujilettea maendeleo yao hasa kutokana na utaratibu wake ambao kwa asilimia mia moja unamshirikisha mwananchi katika kuamua na kupanga miradi wanayoitaka. Nazipongeza sana kamati mbali mbali za wataalamu kutoka taasisi za serikali kwa namna zilivyoshirikiana na wanajamii katika kuibua miradi yao. Vile vile Kamati ya Taifa “*Steering Committees*” zote Unguja na Pemba kwa kazi zao kubwa katika utekelezaji wa miradi hii.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2006 hadi Januari, 2009, jumla ya miradi 108 yenye thamani ya shilingi 2.6 imekamilika kutekelezwa Unguja na Pemba katika sekta mbali mbali. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Sekta ya Elimu Miradi 28.
- (b) Sekta ya Afya miradi 4.
- (c) Sekta ya Maji 26.
- (d) Sekta ya Kilimo, Mifugo na Misitu miradi 38.
- (e) Sekta ya Mawasiliano, miradi 8
- (f) Sekta ya Biashara miradi 5

Mgawano wa miradi hiyo katika Wilaya ilikuwa kama ifuatavyo:-

Unguja -	Wilaya ya Magharibi	Miradi 12
	Wilaya ya Kati	Miradi 12
	Wilaya ya Kaskazini “A”	Miradi 8
	Wilaya ya Kusini	Miradi 7
	Wilaya ya Kaskazini “B”	Miradi 5
	Wilaya ya Mjini	Miradi 5
Pemba -	Wilaya ya Chake Chake	Miradi 16
	Wilaya ya Wete	Miradi 17
	Wilaya ya Micheweni	Miradi 14
	Wilaya ya Mkoani	Miradi 12

Mhe. Spika, jumla ya miradi 136 yenye thamani ya shilingi 2.2 inaendelea kutekelezwa Unguja na Pemba. Miradi hii inahusu Sekta za Uvuvi, ukulima wa mwani, kusokota kamba, ujenzi wa masoko ya kuuzia samaki, kilimo na ufugaji. Vile vile jumla ya miradi 125 ya UKIMWI ilipatiwa fedha jumla shilingi 2.6 katika shehia mbali mbali Unguja na Pemba. Mgawanyo katika Wilaya ulikuwa kama ifuatavyo:-

Unguja -	Wilaya ya Mjini	Miradi 20
	Wilaya ya Kaskazini “A”	Miradi 15
	Wilaya ya Magharibi	Miradi 13
	Wilaya ya Kati	Miradi 13
	Wilaya ya Kaskazini “B”	Miradi 11
	Wilaya ya Kusini	Miradi 6
Pemba -	Wilaya ya Chakechake	Miradi 16
	Wilaya ya Wete	Miradi 11
	Wilaya ya Mkoani	Miradi 10
	Wilaya ya Micheweni	Miradi 10

#### **MATATIZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ya TASSAF**

- (i) Kuna upungufu wa wataalamu wa kusimamia miradi ya TASSAF katika baadhi ya shehia na maeneo.
- (ii) Kuna ushirikiano mdogo kati ya taasisi mbali mbali zinazohusika na miradi hiyo ya maendeleo.
- (iii) Ari ya kuchangia miradi ya TASSAF imepungua katika baadhi ya maeneo. Jukumu la wananchi kuchangia huwaelemea wananchi wachache hasa

- Wajumbe wa Kamati za Usimamizi na Viongozi  
wa Maeneo.
- (iv) Wasimamizi wakuu wa miradi wana uwezo  
mdogo wa kupanga na kusimamia mipango ya  
maendeleo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali utekelezaji wa miradi utakamilika mwaka huu wa 2009. Serikali inatarajia kwamba wanajamii wataitunza na kuienzi miradi hiyo kwa faida ya vizazi vijavyo. Nawaomba wanasiwa, viongozi na wataalamu mbali mbali kuwa karibu na wananchi na kutoa ushauri na miongozo itakayosaidia kuendeleza miradi hiyo hasa kwa shehia zilizopata miradi ya kudumu.

Mhe. Spika, tatizo la ugonjwa wa UKIMWI bado unaendelea na utaendelea kwa situ nyingi zijazo kusababisha athari kubwa sana za kijamii na maendeleo ya taifa letu. Kwa kuwa UKIMWI unawaathiri zaidi vijana shababi wenye nguvu wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45. Tunapaswa kudhibiti ili tusiendelee kupoteza nguvu kazi muhimu sana ya taifa letu inayoangamia kutokana na maradhi ya UKIMWI. Ugonjwa huu unasababisha madhila makubwa katika familia hasa pale familia inapopoteza mzazi au mlezi. UKIMWI unaleta huzuni kubwa kwa watoto wanaofiliwa na walezi wao. Hali hii huwakosesha malezi bora na matunzo. Vile vile UKIMWI huongeza gharama za matibabu kwa wagonjwa. Jambo hili husababisha matatizo makubwa ya kiuchumi hasa kwa nchi zenye rasilimali chache kama Zanzibar.

Mhe. Spika, taarifa zinaonesha kuwa maambukizi ya maradhi ya UKIMWI yanaongezeka kwa kasi kwa sababu wananchi wengi bado hawajakubali kubadili tabia. Kila kukicha yanatokea maambukizi mapya kwa sababu makundi hatarishi katika jamii yanaendelea kufanya vitendo vinavyoongeza maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kwa mfano, wataalamu wa afya wanatunaelezwa kuwa asilimia 17 ya watumiaji wa madawa ya kulevyia iliambukizwa UKIMWI mwaka 2007. Asilimia 15 ya wanaume wanaofanya vitendo kinyume na maumbile na makahaba asilimia 10 pia wameambukizwa virusi vya UKIMWI. Hizi sio takwimu ndogo hata kidogo zinatisha.

Mhe. Spika, kutokana na viashiria hivi ni dhahiri kuwa maambukizi ya UKIMWI yanaongezeka pamoja na kwamba kiwango cha maambukizi bado ni asilimia 0.6. Takwimu hizi zisitupe matumaini na faraja kwa

sababu zinowahusu watu waliopimwa tu wako wengi bado. Inawezekana kuna watu wengi zaidi wanaishi na virusi vya UKIMWI bila ya wao wenyewe kujua. Kwa hivyo, naendelea kutoa wito kwa wananchi tubadili tabia zetu kwa kuchukua hadhari kubwa, zikiwemo za kujiepusha na zinaa na kupima ili kujua afya zetu. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI. Kwanza, serikali inawaelimisha wananchi juu ya athari za UKIMWI. Pili, serikali inawashauri wananchi wanaoshindwa kujizuia watumie vifaa vitakavyowasadid a kujikinga na maambukizi ya UKIMWI. Ikiwezekana pengine njia sahihi zaidi ni kuzuia hisia hizo za mwili. Tatu, serikali inatoa huduma bure za upimaji wa damu katika hospitali na vituo vya afya. Nne, serikali inatoa dawa za kurefusha maisha Unguja na Pemba.

Kutokana na ukubwa wa tatizo la UKIMWI bado juhudhi hizi za serikali hazijaleta mafanikio tuliyoyatarajia. Ipo haja ya kuendelea kuwaelimisha wananchi wajikinge na UKIMWI kwani waswahili husmea “kinga ni bora kuliko tiba”. Sisi viongozi wa kisiasa Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wabunge na Wawakilishi tuna nafasi kubwa sana ya kuwaelimisha wananchi kwa sababu tuna ushawishi mkubwa sana kwa watu tunaowaongoza. Viongozi wa dini nao kwa upande wao wanasilizwa sana na wanaaminiwa sana na waumini wao. Kwa hivyo, naomba nao waendelee kuwakumbusha waumini wao juu ya athari na namna ya kujikinga na virushi vya UKIMWI.

Mhe. Spika, inawezekana tutimize wajibu wetu.

Baada ya kusema hayo basi, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 25 Machi, 2009 saa 3.00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri Kiongozi kwa hotuba hiyo ya ufungaji tunashukuru sana kwa hotuba hiyo. Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri Kiongozi kuahirisha mukutano huu hadi siku ya Jumatano tarehe 25

Machi, 2009 saa 3:00 asubuhi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 11:55 jioni Baraza lilahirishwa hadi tarehe 25/03/2009 saa 3:00  
asubuhi)*